# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2019

**Kimetolewa na:**
**Baraza la Mitihani la Tanzania,**
**S. L. P 2624,**
**Dar es Salaam.**

**Mei, 2020**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2019

Kimetolewa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P 2624,
Dar es Salaam.

**Mei, 2020**

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................................ vi

ORODHA YA CHATI ................................................................................ vii

ORODHA YA VIELELEZO........................................................................ ix

SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU ....................1

1.1 Utangulizi ...........................................................................................1
1.2 Sampuli ya Upimaji..............................................................................1
1.3 Mipaka ya Upimaji ...............................................................................2
1.4 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji .....................................................2
1.5 Uchambuzi wa Takwimu za Upimaji wa Stadi za KKK 2020 ..............2

SURA YA PILI ............................................................................................4

UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA .............................................................4

2.1 Utangulizi ...........................................................................................4
2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma .......................4
2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kusoma .....................................5
2.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi..................................................6
2.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kusoma Maneno ...........................................6
2.4.1.1 Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma kila Neno ..............................9
2.4.2 Swali la 2: Umahiri wa Kujenga Ufahamu katika Kusoma ................12
2.4.2.1 Utendaji wa Wanafunzi katika kila Kipengele cha Ufahamu .............16
2.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo na Jinsi (wavulana/wasichana) .......................................18
2.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa ................................18
2.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo 20
2.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi .............20
2.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kusoma............................21

SURA YA TATU.........................................................................................22

UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA ..........................................................22

3.1 Utangulizi .........................................................................................22
3.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuandika....................22
3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuandika kwa Kila Umahiri ......22
3.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi................................................23
3.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kutambua Picha na Kuandika Jina la Picha Husika ..............................................................................................23

3.4.1.1 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi katika Kila Neno ................28
3.4.2 Swali la 2: Kupigia Mstari Maneno Yaliyoandikwa kwa Herufi Ndogo ........................................................................................33
3.4.3 Swali la 3: Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi ........................................................................37
3.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo (Mijini/Vijijini) na Jinsi (Wavulana/Wasichana). ..................................................................42
3.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa ...............................42
3.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Mahali Shule Zilipo .........................................................44
3.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa kuzingatia Jinsi..............44
3.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuandika .........................45

SURA YA NNE ..........................................................................................47

UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU ..........................................................47

4.1 Utangulizi ..........................................................................................47
4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji .......................................................47
4.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuhesabu ................................48
4.4 Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu...................................48
4.5 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi...............................................49
4.5.1 Umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mfululizo wa Namba 49
4.5.2 Umahiri wa Wanafunzi katika Kujumlisha........................................53
4.5.3 Umahiri wa Wanafunzi katika Kutoa ................................................55
4.5.4 Umahiri wa Wanafunzi katika Kufumbua Mafumbo ..........................56
4.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi .............62
4.6.1 Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia Jinsi katika Upimaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo .....................................63
4.6.2 Ulinganifu wa Jinsi katika Upimaji wa Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa 64
4.7 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo.......................................................................................................65
4.7.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini .........................................65
4.7.2 Ulinganifu wa Utendaji katika Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa Namba kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini .............................66
4.7.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo Kimikoa.........................................67

4.7.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Upimaji wa Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa Namba kwa Kuzingatia Mikoa ........................69
4.7.5 Ulinganifu wa Wanafunzi kwa Ujumla Kimikoa................................71
4.8 Muhtasari wa Uchambuzi Katika Stadi ya Kuhesabu .......................73

SURA YA TANO ..........................................................................................75

HALI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KKK SHULENI............................75

5.1 Taarifa za Shule kwa Ujumla..........................................................75

5.2 Hali ya Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia .........................75

5.3 Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji KKK.....................................76

5.4 Vikwazo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK...............77

SURA YA SITA ...........................................................................................79

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.................................................................79

6.1 Hitimisho .......................................................................................79
6.2 Mapendekezo..................................................................................80

Kiambatisho Na. 1: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kusoma............................82

Kiambatisho Na. 2. Skeli ya Upimaji Stadi ya Kusoma .................................91

Kiambatisho Na. 3: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika..........................98

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na.1: Utendaji wa Wanafunzi Waliofanya Upimaji 2019 kwa kila Stadi…………………… ........................................................ 3
Jedwali Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ...................... 6
Jedwali Na. 3:Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali ya Ufahamu .... 12
Jedwali Na.4: Utendaji wa Jumla wa Stadi ya Kuandika............................... 23
Jedwali Na.5: Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu.......................... 48
Jedwali Na.6: Maswali ya Kujumlisha ........................................................... 53
Jedwali Na.7: Maswali ya Kutoa ................................................................... 55
Jedwali Na.8: Maswali ya Mafumbo.............................................................. 56
Jedwali Na.9: Hali ya Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia ............................ 75
Jedwali Na. 10: Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji................................. 76
Jedwali Na. 11: Vikwazo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK ... 77

## ORODHA YA CHATI


Chati Na. 1: Utendaji wa wanafunzi katika kusoma kila neno. ....................... 10

Chati Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kila Kipengele cha Swali la 2. .. 17

Chati Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi Kimkoa ............................................... 19

Chati Na. 4: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Wanaosoma Shule za Mjini na Wanaosoma Shule za Vijijini. .................................... 20

Chati Na. 5: Ulinganifu wa Utendaji Kati ya Wavulana na Wasichana .......... 21

Chati Na. 6: Utendaji wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha. .......... 24

Chati Na. 7: Utendaji wa wanafunzi katika kutambua maneno yenye herufi ndogo. ........................................................................ 34

Chati Na. 8: Utendaji wa wanafunzi katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. .................................................. 38

Chati Na. 9: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa. ......................... 43

Chati Na. 10: Ulinganifu wa Utendaji wa wanafunzi kwa shule za mjini na vijijini. ........................................................................ 44

Chati Na. 11: Ulinganifu wa Utendaji wa Jinsi. ............................................. 45

Chati Na. 12: Asilimia ya wanafunzi walioweza kutambua namba inayokosekana kwenye mfululizo wa namba katika kila swali. . 50

Chati Na. 13: Asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali ya kujumlisha namba. ................................................................ 54

Chati Na. 14: Asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali ya kutoa namba.......................................................................... 56

Chati Na. 15: Asilimia ya wanafunzi waliofumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa. ........................................................................ 57

Chati Na.16: Matokeo ya jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa wavulana na wasichana. ........................................................................ 63

Chati Na. 17: Matokeo ya jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa Jinsi. ............ 64

Chati Na. 18: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini. ........................................................................ 65

Chati Na. 19: Ulinganifu wa utendaji kwa shule za mijini na vijijini katika kujibu

maswali ya kujumlisha na kutoa. ........................................... 66
Chati Na. 20: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mikoa. .. 68
Chati Na. 21: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mikoa. ... 70
Chati Na. 22: Ulinganifu wa jumla wa utendaji wa wanafunzi kimikoa……… 73

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Sampuli ya jibu sahihi la mmoja wa wanafunzi katika swali la 1. .......... 7
Kielelezo Na. 2: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyesoma maneno kumi (10) kati ya maneno hamsini (50) kwa dakika moja. .......... 7
Kielelezo Na. 3: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kusoma neno hata moja katika swali hili. .......... 8
Kielelezo Na. 4: Sampuli ya jibu la mwanafunzi mwenye utendaji wa wastani katika swali la 1. .......... 8
Kielelezo Na. 5: Sampuli ya jibu sahihi la wanafunzi kwa swali la 1. .......... 9
Kielelezo Na. 6: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani katika swali la 2. .......... 13
Kielelezo Na. 7: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 2. .......... 14
Kielelezo Na. 8: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 2.......... 14
Kielelezo Na. 9: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji mzuri katika swali la 2. .......... 15
Kielelezo Na. 10: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji mzuri katika swali la 2. .......... 16
Kielelezo Na. 11: Sampuli ya jibu baya.......... 25
Kielelezo Na. 12: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani. .......... 26
Kielelezo Na. 13: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri. .......... 27
Kielelezo Na. 14: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.. 28
Kielelezo Na. 15 (a): Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepigia mstari maneno yote.......... 35
Kielelezo Na. 16: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani. 36
Kielelezo Na. 17: sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.......... 36

Kielelezo Na.18: sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana. .................... 37
Kielelezo Na.19: Majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. .................... 39
Kielelezo Na. 20: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani. .................... 40
Kielelezo Na. 21: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri. .................... 41
Kielelezo Na. 22: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana. 41
Kielelezo Na. 23: Majibu ya mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi namba zinazokosekana katika maswali yote. .................... 51
Kielelezo Na. 24: Majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi swali la 1, 2 na 4. .................... 52
Kielelezo Na. 25: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu swali 1 tu. .................... 52
Kielelezo Na. 26: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa. .................... 59
Kielelezo Na. 27: Sampuli ya kazi ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali ya mafumbo. .................... 60
Kielelezo Na. 28: Sampuli ya majibu mwanafunzi aliyeshindwa kufumbua mafumbo yote. .................... 62

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania lilifanya Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Pili mwaka 2019. Upimaji huo ulifanyika ili kutathmini umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi hizo. Upimaji ulifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo jumla ya shule 524 za Msingi kutoka katika Halmashauri zote ziliteuliwa kushiriki. Vilevile, kati ya shule 2 hadi 5 ziliteuliwa kutoka katika kila Halmashauri kwa kuzingatia mazingira ya kijijini na mjini.

Baraza la Mitihani liliandaa zana za upimaji kwa Stadi zote tatu. Shule zote 524 zilitumia karatasi za maswali kwa Stadi ya Kuhesabu na Kuandika. Aidha, jumla ya shule 482 zilitumia Skeli ya Upimaji kwa Stadi ya Kusoma na Kuhesabu ambazo zilifanyika kwa njia ya mdomo wakati shule 42 zilitumia Vishikwambi katika upimaji huo. Pia, Mwalimu Mkuu na Wasimamizi walioteuliwa kusimamia Upimaji walijaza dodoso kuhusu hali ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK.

Jumla ya wanafunzi 35,358 walisajiliwa kufanya upimaji wa Stadi za KKK ambapo wanafunzi 28,816 walifanya upimaji. Hivyo, wanafunzi 6,542 hawakufanya upimaji huo kutokana na sababu mbalimbali.

Uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi unaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji katika stadi zote tatu ulikuwa mzuri (69.02%). Stadi ya Kuandika ilikuwa na utendaji wa juu zaidi kwani asilimia 75.20 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na Stadi ya Kusoma (74.80%) na Kuhesabu (64.20%).

Taarifa hii imegawanyika katika sura sita. Sura ya Kwanza ni Utangulizi na Sura ya Pili, Tatu na ya Nne zinahusu Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, mtawalia. Sura ya Tano inaelezea Uchambuzi wa Taarifa za Usimamizi na Sura ya Sita ni Mapendekezo na Hitimisho.

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa hii ili kutoa mrejesho kwa wadau wa Elimu juu ya ubora wa wanafunzi na changamoto zao katika Stadi za KKK.

Hivyo, inatarajiwa kuwa, kutokana na uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi, wadau wa Elimu wataweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK ili kuboresha umahiri wa wanafunzi katika kumudu Stadi hizo.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# SURA YA KWANZA
# SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU

## 1.1 Utangulizi

Baraza la Mitihani la Tanzania lilifanya upimaji kwa wanafunzi wa Darasa la Pili katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) tarehe **31/01/2020** na tarehe **01/02/2020** ili kubaini uwezo wa wanafunzi katika stadi hizo. Upimaji huu ulifanyika kwa wanafunzi wa Darasa la Tatu 2020 waliomaliza mtaala wa Darasa la Kwanza na la Pili mwaka 2019.

Katika Stadi ya Kusoma, wanafunzi walipimwa umahiri wa kutambua sauti, herufi, kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha, umakini na kwa haraka na kujenga ufahamu wa kujibu maswali na kukuza msamiati. Aidha, katika Stadi ya Kuandika, wanafunzi walipimwa umahiri wa kuunda maneno kwa kutumia picha, kubainisha maneno yaliyoundwa kwa herufi kubwa na ndogo, kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi mahali panapostahili. Katika Stadi ya Kuhesabu, wanafunzi walipimwa umahiri wa kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba zinazoongezeka na zinazopungua, kujumlisha na kutoa namba zisizozidi 999 na kufumbua mafumbo.

## 1.2 Sampuli ya Upimaji

Upimaji ulifanyika katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ambayo ni: Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga. Aidha, jumla ya halmashauri 186 za mikoa yote zilishiriki upimaji huo ambapo katika kila halmashauri shule ziliteuliwa kwa kuzingatia maeneo ya mijini na vijijini. Kati ya Shule 2 hadi 5 zinazotumia mfumo wa lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia ziliteuliwa kwa kila Halmashauri hivyo kufanya idadi ya shule zilizopimwa kuwa 524. Jumla ya wanafunzi 28,816 walifanya upimaji wa Stadi ya Kusoma, wanafunzi 28,816 walifanya Stadi ya Kuandika na jumla ya wanafunzi 28,022 walipimwa katika Stadi ya Kuhesabu. Mahudhurio ya wanafunzi katika upimaji huo yalitofautiana kati ya stadi moja na nyingine kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo; utoro, ugonjwa, mvua na uhamisho.

## 1.3 Mipaka ya Upimaji

Katika Upimaji huu, baadhi ya mipaka ya upimaji ilijitokeza katika sampuli iliyotumika. Miongoni mwa mipaka hiyo ni pamoja na kikwazo cha muda na hali ya hewa. Njia ya sampuli nasibu ilitumika kuteua shule za kufanya upimaji, ambapo shule 524 tu ziliteuliwa kati ya 16,000 za Tanzania bara. Hata hivyo, Shule zilizoteuliwa hazikuhusisha shule za binafsi zinazotumia lugha ya kiingereza kufundishia na kujifunzia. Aidha, data zilizotumika kukokotoa utendaji wa wanafunzi katika kila stadi hazikufanyiwa uzani (weighting), hivyo uchambuzi ulifanyika kwa kutumia sampuli halisi.

Vilevile, mafunzo kwa wawezeshaji na wasimamizi yalipangwa kufanyika kwa siku nne. Hata hivyo, kutokana na kikwazo cha muda, wawezeshaji walipewa mafunzo kwa siku tatu wakati wasimamizi walipewa mafunzo kwa siku nne. Pia, ufanyikaji wa upimaji uliathirika kutokana na hali ya hewa kuwa ya mvua ya mafuriko. Hivyo, kusababisha kubadilisha baadhi ya shule zilizokuwa zimeteuliwa kwa ajili ya kufanya upimaji.

## 1.4 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji

Zana zilizotumika kwenye upimaji ni: karatasi za maswali ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (ona Kiambatisho.Na.1 hadi 4). Maswali yaliyotungwa kwa kila stadi yalilenga kupima umahiri wa wanafunzi kwa kuzingatia viwango vya utendaji. Aidha, madodoso yaliandaliwa kwa ajili ya wasimamizi na walimu wakuu ili kupata taarifa kuhusu walimu wanaofundisha stadi za KKK, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

## 1.5 Uchambuzi wa Takwimu za Upimaji wa Stadi za KKK 2020

Uchambuzi wa takwimu katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulifanyika ili kufahamu na kutoa taarifa kuhusu umahiri wa wanafunzi katika kila stadi. Umahiri huo ulipimwa kwa kuzingatia viwango vya utendaji ambapo alama 0 – 12 ni utendaji hafifu, 13 – 25 utendaji wa wastani, 26 – 37 utendaji mzuri na 38 – 50 utendaji mzuri sana. Aidha, takwimu za uchambuzi wa viwango vya utendaji kwa kila stadi zimewasilishwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1: Utendaji wa Wanafunzi Waliofanya Upimaji 2019 kwa kila Stadi**

| Stadi | Idadi ya Wanafunzi Waliofanya Upimaji | Wanafunzi waliokuwa na Utendaji wa Wastani hadi Mzuri sana | |
|---|---|---|---|
| | | Idadi | Asilimia |
| Kusoma | 28,816 | 21,554 | 74.80 |
| Kuandika | 28,816 | 21,670 | 75.20 |
| Kuhesabu | 28,022 | 17,991 | 64.20 |

Wakati wa uchambuzi, sampuli za majibu ya wanafunzi zilitumika ili kuonesha umahiri wao katika utendaji na changamoto walizokuwa nazo katika kila stadi. Pia, uchambuzi wa takwimu ulihusisha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia jinsi, mahali shule ilipo na katika ngazi ya Mkoa.

# SURA YA PILI

## UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA

### 2.1 Utangulizi

Upimaji wa Stadi ya Kusoma umefanyika ili kubaini uwezo wa wanafunzi katika kusoma kifungu cha maneno hamsini kwa ufasaha na kwa kasi inayotakiwa. Aidha, kifungu hicho kilipima uelewa wao wa kujibu maswali ya ufahamu. Uchambuzi umezingatia kigezo cha utendaji wa wanafunzi katika kusoma kifungu cha maneno na kujibu maswali ya ufahamu. Umahiri wa wanafunzi katika swali la kwanza ulitegemea idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza kusoma kwa ufasaha ndani ya dakika moja. Katika swali la pili, umahiri wa mwanafunzi ulipimwa kwa kuzingatia uwezo wake wa kusoma kifungu cha maneno, kuelewa na kutafsiri alichokisoma kisha kujibu maswali ya ufahamu kwa njia ya mdomo. Aidha, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi umefanyika kwa kuzingatia Mikoa, mahali shule ilipo (mijini/vijijini) na jinsi (wavulana /wasichana).

### 2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma

Karatasi ya upimaji wa stadi ya Kusoma ilikuwa na maswali mawili. Maswali hayo yaliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walipimwa kwa karatasi ya upimaji (skeli ya upimaji) katika Halmashauri 175 na Halmashauri 11 walipimwa kwa kishikwambi (tablet). Swali la kwanza lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma kifungu chenye maneno hamsini (50) kwa haraka na ufasaha kwa muda wa dakika moja na swali la pili lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo baada ya kusoma kifungu cha maneno.

Upimaji kwa kutumia karatasi ya upimaji (skeli ya upimaji) ulifanyika kwa muda wa dakika kumi (10) kwa kila mwanafunzi. Dakika moja (1) ilitumika kumpima mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha na dakika tatu (3) zilitumika kusoma tena kifungu hicho ili kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo. Vilevile, msimamizi alitumia dakika sita (6) kwa ajili ya kujaza alama za mwanafunzi wakati anasoma, kuuliza maswali ya ufahamu, kukokotoa na kujaza jumla ya alama za mwanafunzi katika skeli ya upimaji kwa maswali yote.

Aidha, upimaji kwa kutumia kishikwambi (tablet) ulitumia muda wa dakika tano (5) kwa kila mwanafunzi. Dakika moja (1) ilitumika kusoma kifungu cha maneno na wakati huo msimamizi alirekodi alama za mwanafunzi kwa kutumia mfumo uliokuwa kwenye kishikwambi ambapo alama hizo

zilidakwa moja kwa moja kwenye mfumo. Vilevile, dakika tatu (3) zilitumika kusoma tena kifungu cha maneno ili kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo. Msimamizi alitumia dakika moja (1) kuuliza maswali ya ufahamu.

### 2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kusoma

Upimaji wa Stadi ya Kusoma ulizingatia viwango vinne (4) vya utendaji ambavyo ni: utendaji mzuri sana, utendaji mzuri, utendaji wa wastani na utendaji hafifu. Katika swali la kwanza, mwanafunzi aliyeweza kusoma maneno 38-50 kwa usahihi ndani ya dakika moja, alikuwa na utendaji mzuri sana, mwanafunzi alikuwa na utendaji mzuri kwa kuweza kusoma maneno 26-37, 13-25 wastani na aliyesoma maneno 0-12 alikuwa na utendaji hafifu.

Ili kupata idadi ya maneno yaliyosomwa na mwanafunzi, msimamizi alitakiwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) Iwapo mwanafunzi alisoma maneno yote kwa ufasaha, msimamizi aliweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho katika kifungu cha maneno.

(b) Iwapo mwanafunzi alishindwa kusoma neno kwa ufasaha, msimamizi aliweka alama ya mkwaju (/).

(c) Iwapo msimamizi aliweka alama ya mkwaju (/) mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kusoma kwa usahihi, alizungushia (Ø) neno hilo.

(d) Iwapo mwanafunzi alishindwa kusoma maneno yote ya sentensi ya kwanza, msimamizi aliweka mkwaju katika maneno hayo kisha kuweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho katika sentensi hiyo. Aidha, msimamizi alihesabia kuwa ni kosa kwa maneno yote yaliyofuata.

(e) Iwapo mwanafunzi alishindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya dakika moja, msimamizi aliweka mabano [ ] kwenye neno la mwisho kusomwa na kuhesabia kosa kwa maneno yote yaliyofuata.

Kigezo cha utendaji wa umahiri wa mwanafunzi katika swali la pili, kilizingatia idadi ya vipengele vya swali ambavyo mwanafunzi alivijibu kwa usahihi baada ya kusoma tena kifungu cha maneno alichokisoma

katika swali la kwanza. Swali lilikuwa na vipengele vitano (5) ambavyo mwanafunzi alitakiwa kuvijibu. Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vitano (5) alikuwa na utendaji mzuri sana, vinne (4) utendaji mzuri, viwili (2) hadi vitatu (3) utendaji wa wastani na aliyejibu kwa usahihi kipengele kimoja (1) au kushindwa vipengele vyote alikuwa na utendaji hafifu.

## 2.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

Jumla ya wanafunzi 35,358 walisajiliwa kufanya upimaji wa Stadi ya Kusoma ambapo kati yao wanafunzi 28,816 (81.15%) walifanya upimaji huo. Wavulana walikuwa 14,010 (48.62%) na wasichana walikuwa 14,807 (51.38%). Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi hao unaonesha kuwa asilimia 74.80 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana na asilimia 25.20 walikuwa na utendaji hafifu.

### 2.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kusoma Maneno

Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma maneno hamsini (50) kwa ufasaha kwa muda wa dakika moja. Utendaji wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwani asilimia 75.12 ya wanafunzi waliweza kusoma maneno 13 hadi 50. Kwa upande mwingine, asilimia 24.88 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu kwa kusoma maneno 0-12. Jedwali Na. 2 linaonesha utendaji wa wanafunzi katika swali hili.

**Jedwali Na.2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 0 – 12 | Hafifu | 7,168 | 24.88 |
| 13 – 25 | Wastani | 6,342 | 22.01 |
| 26 – 37 | Mzuri | 6,183 | 21.46 |
| 38 – 50 | Mzuri Sana | 9,123 | 31.66 |
| **Jumla** | | **28,816** | **100** |

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 9,123 sawa na asilimia 31.66 walikuwa na utendaji mzuri sana kwani waliweza kusoma kwa ufasaha maneno 38 hadi 50 ambayo ni zaidi ya robo tatu ya maneno yote yaliyotakiwa kusomwa. Kielelezo Na. 1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana kwani alisoma kwa ufasaha maneno yote hamsini.

Tina na Subira ni marafiki.
Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka [hospitali.]

**Kielelezo Na. 1:** Sampuli ya jibu sahihi la mmoja wa wanafunzi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1, mwanafunzi alionesha uwezo wa kusoma maneno yote hamsini (50) kwa ufasaha. Mwanafunzi huyo alisoma kifungu cha maneno ndani ya dakika moja (1) kama ilivyoelekezwa.

Vilevile, wanafunzi 7,169 sawa na asilimia 24.88 walikuwa na utendaji hafifu ambapo asilimia 36.38 waliweza kusoma neno 1 hadi maneno 12 na asilimia 63.62 walishindwa kusoma hata neno moja kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2 na 3, mtawalia.

Tina na Subira ni marafiki.
Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina (shida) kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 2**: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyesoma maneno kumi (10) kati ya maneno hamsini (50) kwa dakika moja.

Katika Kielelezo Na. 2, mwanafunzi alisoma maneno kumi (10) kwa usahihi. Idadi hiyo ya maneno aliyoweza kusoma inaonesha kuwa mwanafunzi huyo alikuwa na utendaji hafifu.

> Tina na Subira ni marafiki.
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 3**: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kusoma neno hata moja katika swali hili.

Katika kielelezo Na. 3, mwanafunzi alishindwa kusoma neno lolote katika kifungu cha maneno alichopewa, hivyo kuwa na utendaji hafifu.

Hata hivyo, wanafunzi 6,342 sawa na asilimia 22.01 waliweza kusoma maneno 13 hadi 25 kwa ufasaha hivyo kuwa na utendaji wa wastani kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4.

> Tina na Subira ni marafiki.
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 4**: Sampuli ya jibu la mwanafunzi mwenye utendaji wa wastani katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 4, mwanafunzi alionesha utendaji wa wastani kwani aliweza kusoma kwa ufasaha maneno ishirini na nne (24). Mwanafunzi huyo alitumia dakika moja katika kusoma maneno

hayo katika kifungu cha maneno.

Kwa upande mwingine, asilimia 21.46 ya wanafunzi waliofanya upimaji wa Stadi ya Kusoma walikuwa na utendaji mzuri kwani waliweza kusoma maneno 26 hadi 37 kwa ufasaha. Idadi ya maneno hayo ni zaidi ya nusu ya maneno yote yaliyotakiwa kusomwa katika swali hili. Kielelezo Na. 5 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.


> Tina na Subira ni marafiki.
> Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe [alikuwa] amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Kielelezo Na. 5**: Sampuli ya jibu sahihi la wanafunzi kwa swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 5, mwanafunzi alimudu kusoma kwa ufasaha maneno thelathini na saba (37) kwa dakika moja. Idadi ya maneno aliyosoma inaonesha utendaji mzuri.

### 2.4.1.1 Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma kila Neno

Wanafunzi walionesha utendaji tofauti katika kusoma maneno kwenye swali la kwanza. Baadhi yao, waliweza kusoma maneno kwa ufasaha na wengine walishindwa kutokana na sababu mbalimbali. Chati Na. 1 inaonesha asilimia ya wanafunzi walioweza kusoma kila neno.




**Chati Na. 1**: *Utendaji wa wanafunzi katika kusoma kila neno.*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kusoma maneno yanayoundwa kwa silabi moja kama vile: *na* (81.71%), *ni* (80.79%) na *cha* (78.98%). Vilevile, maneno yaliyoundwa na silabi zenye konsonanti moja na irabu yalisomwa kwa ufasaha zaidi kuliko yaliyoundwa na silabi zenye konsonanti mwambatano. Maneno hayo ni pamoja na: *Tina* (77.50%), *kina* (77.07%), *kijiji* (75.23%) na *siku* (73.11%).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi walishindwa kusoma baadhi ya maneno kwa usahihi kutokana na sababu mbalimbali. Maneno hayo ni kama: *Ng'alo* (31.05%), *Subira* (57.41%) na *Mara* (38.87%). Wanafunzi hao walishindwa kusoma neno 'Ng'alo' kwa sababu limeundwa na sauti ya konsonanti *ng*' (king'ong'o) ambayo hutamkwa kwa kutoa hewa kwa njia ya pua. Wengi wao walitamka sauti hiyo kwa kutoa hewa kwa njia ya mdomo badala ya njia ya pua. Hivyo, walitamka neno *Ngalo* badala ya *Ng'alo*.

Aidha, baadhi ya wanafunzi walishindwa kusoma neno "Mara" na "Subira" kwa sababu walishindwa kutofautisha sauti 'r' na sauti 'l' hivyo, walitamka sauti 'l' badala ya 'r'. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha sauti hizo kutokana na athari za lugha za asili katika lugha ya pili (lugha ya Kiswahili).

Vilevile, sauti 'r' na 'l' ni sauti za vilainisho ambazo zinatamkwa kwenye ufizi bila kuzuia hewa. Sauti 'r' inapotamkwa ncha ya ulimi hugusana na sehemu ya nyuma ya ufizi wakati huo pembe za ulimi hugusana na kingo za kaakaa. Sauti 'l' inapotamkwa ncha ya ulimi huinuliwa na kugusana na ufizi na kusababisha hewa kupita kwenye pembe za ulimi. Hivyo, ilikuwa changamoto kwa baadhi ya wanafunzi kutofautisha namna ya kutamka sauti hizo ambazo zinatamkiwa eneo moja la matamshi.

Kwa upande mwingine, asilimia 80.97 ya wanafunzi walishindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya muda wa dakika moja. Wengi wao waliishia kusoma neno *kupiga* ambalo ni neno la thelathini na tano (35) katika kifungu hicho. Maneno mengine waliyoshindwa kusoma ndani ya muda uliopangwa ni: *kelele* (39.58%), *kumbe* (36.63%), *alikuwa* (35.98%), *amechomwa* (32.42%), *na* (33.50%), *mwiba* (31.50%), *Hatimaye* (27.72%), *Subira* (22.72%), *alishindwa* (24.01%), *kubeba* (23.50%), *ndoo*

(22.92%), *Wazazi* (20.49%), *wake* (19.95%), *walimpeleka* (17.98%) na *hospitali* (15.82%). Kwa hiyo, wanafunzi wengi waliweza kusoma kwa ufasaha lakini sio kwa kasi inayotakiwa ambapo wanafunzi wote walisoma maneno 26 kwa wastani kwa muda wa dakika moja.

### 2.4.2 Swali la 2: Umahiri wa Kujenga Ufahamu katika Kusoma

Swali la pili lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kusoma kifungu cha maneno, kukielewa na kujibu maswali ya ufahamu kwa mdomo. Swali lilikuwa na vipengele vitano vinavyotokana na kifungu hicho ambacho kilitakiwa kusomwa kwa muda wa dakika tatu. Kifuatacho ni kifungu cha maneno alichotakiwa kusoma mwanafunzi na kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho kwa mdomo.

**Kifungu cha Maneno**

Tina na Subira ni marafiki. Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 20,112 (69.79%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Wanafunzi hao waliweza kujibu kati ya vipengele viwili hadi vitano vya swali hili kwa usahihi. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya utendaji wa wanafunzi katika swali la pili.

**Jedwali Na. 3**: **Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali ya Ufahamu**

| Idadi ya Vipengele | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 1 | Hafifu | 8,704 | 30.21 |
| 2-3 | Wastani | 9,226 | 32.02 |
| 4 | Mzuri | 6,027 | 20.91 |
| 5 | Mzuri sana | 4,859 | 16.86 |
| **Jumla** | | **28,816** | **100** |

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa asilimia 32.02 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani. Wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele viwili hadi vitatu vya swali kwa

usahihi. Kielelezo Na. 6 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? (Subira) | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? (Ng'alo) | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? (Kisimani) | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? (Kata) | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? (Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa) | 5 | 0 |
| Jumla ya Alama | | 15 | |

**Kielelezo Na. 6**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 6, mwanafunzi alionesha umahiri wa wastani katika kujibu maswali ya ufahamu. Utendaji wa wastani wa mwanafunzi huyo umetokana na kujibu kwa usahihi vipengele vitatu (3) vya swali hili. Aidha, mwanafunzi huyo aliweza kujibu kipengele cha 5 cha swali kilichopima umahiri wa ngazi ya juu zaidi ya kufikiri.

Hata hivyo, wanafunzi 8,704 (30.21%) walikuwa na utendaji hafifu. kati yao, wanafunzi 1,955 sawa na asilimia 22.45 waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu kati ya vitano (5). Kielelezo Na. 7 kinaonesha sampuli ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu.

Maswali na Majibu

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? (Subira) | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? (Ng'alo) | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? (Kisimani) | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? (Kata) | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? (Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa) | 5 | 0 |
| | Jumla ya Alama | 5 | |

**Kielelezo Na. 7:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 7, mwanafunzi alijibu kipengele kimoja tu na kuwa na utendaji hafifu.

Aidha, wanafunzi 6,750 (77.56%) walishindwa kujibu kipengele hata kimoja cha swali kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.8.

Maswali na Majibu

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? (Subira) | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? (Ng'alo) | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? (Kisimani) | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? (Kata) | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? (Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa) | 5 | 0 |
| | Jumla ya Alama | 0 | |

**Kielelezo Na. 8**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji hafifu katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 8, mwanafunzi alishindwa kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote vitano vya swali hili, hivyo kuwa na utendaji hafifu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 20.91 ya wanafunzi waliweza kujibu vipengele vinne (4) vya swali kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji mzuri kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 9.

Maswali na Majibu

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |
| | Jumla ya Alama | 20 | |

**Kielelezo Na. 9:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji mzuri katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 9, mwanafunzi alijibu kwa usahihi vipengele vinne (4) hivyo kuwa na utendaji mzuri. Majibu hayo yanaonesha kuwa mwanafunzi huyo alielewa vizuri kifungu cha maneno, hivyo kujibu maswali yaliyopima nyanja ya maarifa na tathmini kwa usahihi. Jambo hili linaonesha kuwa wanafunzi wa kundi hili walikuwa na uelewa wa hali ya juu katika kusoma, kutafsiri walichosoma na kujibu maswali kwa usahihi.

Vilevile, wanafunzi 4,859 (16.86%) walijibu vipengele vyote vitano vya swali kwa usahihi hivyo kuwa na utendaji mzuri sana. Kielelezo Na.10 kinaonesha sampuli ya majibu yao katika swali la pili.


| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? (Subira) | ⑤ | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? (Ng'alo) | ⑤ | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? (Kisimani) | ⑤ | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? (Kata) | ⑤ | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? (Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa) | ⑤ | 0 |
| | Jumla ya Alama | 25 | |

**Kielelezo Na. 10:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi mwenye utendaji mzuri katika swali la 2.

Kielelezo Na. 10 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitano katika swali hili. Mwanafunzi huyo alionesha uwezo mkubwa katika stadi za ufahamu kwa kupata alama ishirini na tano (25).

### 2.4.2.1 Utendaji wa Wanafunzi katika kila Kipengele cha Ufahamu

Katika swali la pili, utendaji wa wanafunzi ulitofautiana katika kujibu vipengele vya swali hilo kutokana na sababu mbalimbali. Pamoja na tofauti hiyo, kwa wastani wanafunzi wote walijibu vipengele viwili kwa usahihi. Kwa ujumla, hii inaashiria kuwa uwezo wa wanafunzi katika kusoma kifungu cha maneno na kujibu maswali ya ufahamu ni wa wastani. Chati Na. 2 inaonesha asilimia ya utendaji wa wanafunzi katika kila kipengele.




**Chati Na. 2**: *Utendaji wa Wanafunzi katika Kila Kipengele cha Swali la 2*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 18,291 (63.47%) waliweza kujibu kipengele cha kwanza cha swali. Swali hilo liliuliza “Rafiki yake Tina anaitwa nani?” Vilevile, asilimia 37.28 ya wanafunzi walijibu kwa usahihi kipengele cha pili kilichouliza “Tina na Subira wanaishi kijiji gani?” Kipengele cha tatu ambacho kiliuliza “Tina na Subira walikwenda wapi?” kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi 17,159 sawa na asilimia 59.54. Asilimia 35.36 ya wanafunzi walijibu kwa usahihi kipengele cha nne kilichouliza “Subira alitumia nini kujaza ndoo yake?” Aidha, jumla ya wanafunzi 17,721 (61.49%) waliweza kujibu kipengele cha tano kwa usahihi kilichouliza “Kwanini Subira alipelekwa Hospitali”.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi wengi (63.47%) walijibu kwa usahihi kipengele cha kwanza kilichouliza “Rafiki yake Tina anaitwa nani?” Wanafunzi hao waliweza kujibu kipengele hicho kwa urahisi kwa sababu kilipima kiwango cha chini cha uwezo wa kufikiria (kukumbuka).

Hata hivyo, kipengele cha nne kilichouliza “Subira alitumia nini kujaza ndoo yake?” kilikuwa na utendaji wa chini ikilinganishwa na vipengele vingine. Wanafunzi wengi walishindwa kujibu kwa usahihi kipengele hicho kwa sababu kilipima kiwango cha juu cha uwezo wa kufikiria.


## 2.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo na Jinsi (wavulana/wasichana)

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kati ya mikoa, mahali shule ilipo (mijini au vijijini), na jinsi (wavulana na wasichana).

Lengo la kufanya ulinganifu huu ni kubaini kama kuna tofauti ya utendaji wa wanafunzi katika makundi hayo ili kuweza kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa

Upimaji wa stadi ya Kusoma kwa mwaka 2020 ulihusisha mikoa yote ya Tanzania Bara. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika ngazi ya mikoa ulizingatia madaraja manne ambayo ni: alama 0-12 utendaji hafifu, 13-25 wastani, 26-37 utendaji mzuri na 38-50 utendaji mzuri sana. Chati Na. 3 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kimikoa.





**Chati Na. 3**: *Utendaji wa Wanafunzi Kimkoa*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi wengi wanaotoka mkoa wa Dar es Saalam wana utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 92.40 katika stadi ya Kusoma. Hata hivyo, katika mkoa wa Kigoma asilimia 59.80 ya wanafunzi wameonesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hivyo, mkoa wa Dar es saalam umekuwa na utendaji wa juu zaidi ukilinganishwa na mikoa mingine. Vilevile, wanafunzi wameonesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 74.80 kitaifa. Kwa ujumla, takwimu hizo zinaonesha kwamba utendaji wa wanafunzi wa Darasa la pili katika Stadi ya Kusoma ni mzuri.

### 2.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo

Jumla ya wanafunzi 28,816 walifanya upimaji wa Stadi ya Kusoma. Kati yao, wanafunzi 10,115 sawa na asilimia 35.10 walitoka shule za mjini na wanafunzi 18,702 sawa na asilimia 64.90 walitoka shule za vijijini. Uchambuzi umefanyika ili kubaini kama kuna utofauti wa utendaji kati ya shule za mjini na vijijini. Chati Na. 4 inaonesha utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mahali shule ilipo.





**Chati Na. 4:** *Utendaji wa Wanafunzi Wanaosoma Shule za Mjini na Wanaosoma Shule za Vijijini.*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi waliopo shule za mjini ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 78.78 ambapo utendaji wa wanafunzi katika shule za vijijini ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 72.64. Hivyo, wanafunzi wanaotoka katika shule za mjini wameonesha utendaji wa juu (ufaulu wa wastani hadi mzuri sana) zaidi kwa asilimia 6.14 wakilinganishwa na wanafunzi wanaotoka katika shule za vijijini.

### 2.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi

Katika upimaji wa Stadi ya Kusoma 2020, wanafunzi 28,816 walipimwa. Wasichana walikuwa 14,807 (51.38%) na wavulana walikuwa 14,010 (48.62%). Uchambuzi wa majibu yao unaonesha kuwa wasichana walikuwa na utendaji wa asilimia 77.82 na wavulana 71.60. Hivyo, wasichana walionesha utendaji mzuri zaidi kwa asilimia 6.22 ikilinganishwa na wavulana. Chati Na. 5

inaonesha ulinganifu wa utendaji kati ya wasichana na wavulana.




**Chati Na. 5**: *Ulinganifu wa Utendaji Kati ya Wavulana na Wasichana.*

## 2.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kusoma

Kwa ujumla, asilimia 74.80 ya wanafunzi walionesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika Stadi ya Kusoma, kwani waliweza kusoma maneno kwa ufasaha na kasi inayotakiwa na kujibu maswali ya ufahamu kwa usahihi. Hata hivyo, asilimia 25.20 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu kwa sababu walishindwa kusoma baadhi ya maneno kwa ufasaha na kasi inayotakiwa, kwa mfano, maneno yaliyoundwa kwa mfuatano wa konsonanti na maneno yaliyoundwa na sauti ‘l’ na ‘r’. Vilevile, wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kusoma kifungu cha maneno, kutafsiri walichokisoma na kujibu maswali ya ufahamu kwa usahihi.

# SURA YA TATU

# UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea Stadi ya Kuandika kwa kuzingatia Muundo wa karatasi ya upimaji, vigezo vya kupima umahiri wa wanafunzi na uchambuzi wa takwimu na majibu ya wanafunzi. Vile vile, sura hii inaeleza maeneo ambayo wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri sana (alama 38 hadi 50), mzuri (alama 26 hadi 37) wastani (alama 13 hadi 25) na hafifu (alama 0 hadi 12). Pia, katika uchambuzi huo, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia mikoa, mahali shule ilipo (mijini/vijijini) na jinsi (Wavulana/Wasichana. Sura hii imehitimishwa kwa muhtasari wa uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji katika Stadi ya Kuandika.

## 3.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuandika

Karatasi ya upimaji wa Stadi ya Kuandika ilikuwa na maswali matatu (03). Swali la kwanza lilikuwa na vipengele 10. Mwanafunzi alipimwa umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha hizo. Vilevile, alipimwa umahiri wa kuunda maneno. Swali la pili lilikuwa na vipengele vitano (5) ambavyo vilimtaka mwanafunzi kupigia mstari maneno 10 yaliyoandikwa kwa herufi ndogo. Lengo lilikuwa kupima umahiri wa mwanafunzi katika kutambua herufi kubwa na ndogo. Swali la tatu lilimtaka mwanafunzi kunakili kifungu cha maneno alichopewa na kuweka alama sahihi za uandishi. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi katika kuandika na kutumia alama za uandishi kwa usahihi.

## 3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuandika kwa Kila Umahiri

Umahiri wa mwanafunzi katika Stadi ya Kuandika ulipimwa kwa kuzingatia viwango vinne (4) vya utendaji ambavyo ni : hafifu, wastani, mzuri na mzuri sana. Katika swali la 1, umahiri wa mwanafunzi ulikuwa hafifu ikiwa aliweza kuandika majina ya picha 0 - 2, wastani majina ya picha 3 - 5, mzuri majina ya picha 6 - 8 na mzuri sana majina ya picha 9 – 10. Umahiri wa mwanafunzi katika kutambua herufi ndogo ulizingatia uwezo wake katika kutambua herufi ndogo. Utendaji ulikuwa hafifu iwapo alipigia mstari maneno 0 – 2, wastani 3 – 5, mzuri 6 – 8 na mzuri sana 9 – 10. Aidha, umahiri wa mwanafunzi wa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi ulizingatia jumla ya alama

alizopata baada ya kunakili kifungu cha maneno na kutumia alama sahihi za uandishi. Iwapo mwanafunzi alinakili maneno na kuweka alama za uandishi na kupata alama 0 – 5 ni utendaji hafifu, wastani 6 – 10, mzuri 11 – 15 na mzuri sana 16 – 20.

## 3.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

Uchambuzi wa takwimu za majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 28,816 walifanya upimaji katika Stadi ya Kuandika. Baadhi yao walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 65.96. Aidha, asilimia 34.04 walikuwa na utendaji hafifu. Jedwali Na. 4 linaonesha utendaji wa jumla katika Stadi ya Kuandika.

**Jedwali Na.4: Utendaji wa Jumla wa Stadi ya Kuandika**


| Umahiri | Viwango vya Utendaji | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu | | Wastani | | Mzuri | | Mzuri Sana | |
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Kuunda Maneno | 6,512 | 22.18 | 5,662 | 19.29 | 9,972 | 33.97 | 7,210 | 24.56 |
| Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo | 12,480 | 42.51 | 2,291 | 7.80 | 3,637 | 12.39 | 10,948 | 37.29 |
| Kunakili Kifungu na Kuweka Alama za Uandishi | 10,982 | 37.41 | 1,912 | 6.51 | 6,944 | 23.65 | 9,518 | 32.42 |

Jedwali Na. 4 linaonesha utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kuandika. Asilimia 77.82, 57.48 na 62.58 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika umahiri wa kuandika majina ya picha, kutambua herufi kubwa na ndogo na kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi, mtawalia. Wanafunzi hao waliweza kutambua picha 3 - 10 na kuandika majina ya picha hizo, kutambua maneno 3 – 10 yaliyoandikwa kwa herufi ndogo, kunakili maneno 6 - 16 na kuweka alama za uandishi 2 – 4 katika kifungu cha maneno.

### 3.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kutambua Picha na Kuandika Jina la Picha Husika

Uchambuzi ulifanyika ili kubaini umahiri wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha. Uchambuzi ulionesha kuwa wanafunzi


22,844 (77.82%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika kutambua picha na kuandika majina ya picha hizo kwa usahihi kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6***: Utendaji wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha***.**

Chati Na. 6 inaonesha utendaji wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha ambapo asilimia 77.82 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha, wanafunzi wachache (22.18%) walikuwa na utendaji hafifu.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 6,512 (22.18%) walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kutambua picha na kuandika kwa usahihi majina yanayowakilisha picha hizo. Baadhi yao waliweza kuandika jina moja hadi mawili tu kutokana na changamoto ya kuunganisha herufi ili kuunda jina sahihi. Pia, wanafunzi wengine waliandika baadhi ya majina kwa kukosea herufi (tahajia). Miongoni mwao walirudia kuchora picha walizopewa badala ya kuandika majina husika na wengine walinakili maelezo ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika maneno ya maelekezo yaliyopo kwenye swali badala ya kutaja majina ya picha husika. Kielelezo Na. 11 kinaonesha sampuli za majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji hafifu.





**Kielelezo Na. 11**: Sampuli ya jibu baya.

Kielelezo Na. 11 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyenakili maelekezo ya swali badala ya kuandika majina yanayowakilisha picha husika.

Kwa upande mwingine, uchambuzi wa upimaji unaonesha kuwa wanafunzi 5,666 (19.29%) walikuwa na utendaji wa wastani. Wanafunzi hao waliweza kutambua picha za vipengele vitatu (3) hadi vitano (5) na kuandika majina ya picha hizo kwa usahihi. Vilevile, walikuwa na changamoto ndogo ya kuunda maneno yenye konsonanti mwambatano. Wanafunzi wengine waliandika baadhi ya majina kwa lugha za asili na wengine walishindwa kuandika maneno yanayoundwa na irabu pekee. Wanafunzi hao waliongeza herufi ambazo ni viyeyusho katika kubainisha jina la picha husika hivyo kuwa na maana tofauti na picha halisi


iliyokusudiwa. Kwa mfano, katika neno “ua” waliongeza kiyeyusho /w/ na kuandika neno “uwa”. Kielelezo Na.12 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.




**Kielelezo Na. 12**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.

Kielelezo Na. 12 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika majina sahihi katika kipengele (a), (d), (f), (g) na (j). Aidha, alishindwa kuandika majina sahihi ya kipengele (b), (c), (e), (h) na (i). Katika kipengele (c) na (e), mwanafunzi alishindwa kuandika kwa usahihi majina yanayoanza na konsonati, ambayo ni nazali “m” aliyoiandika kwa kuongeza irabu “u” hivyo kuandika neno “muguu” na “mupira” badala ya “mguu” na “mpira” mtawalia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 9,972 (33.97%) walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi hao walitambua baadhi ya picha na waliandika majina ya picha hizo kwa usahihi (majina 6 hadi 8). Kielelezo Na. 13 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.




**Kielelezo Na. 13**: Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.

Kielelezo Na. 13 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri, japokuwa alishindwa kuandika majina sahihi katika vipengele (a), (c), (e) na (h).

Vilevile, wanafunzi 7,210 (24.56%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi hao walitambua picha zote na kuandika majina ya picha hizo kwa usahihi kwa sababu walikuwa na umahiri mzuri sana katika kuunda maneno hivyo, kuandika majina yote kwa usahihi. Kielelezo Na. 14 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.




**Kielelezo Na. 14:** Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana**.**

Kielelezo Na. 14 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika majina ya vipengele vyote kwa usahihi kutokana na umahiri mzuri aliokuwa nao katika kuunda maneno.

### 3.4.1.1 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi katika Kila Neno

(a) **Chura**

Wanafunzi 15,307 (52.14%) walishindwa kutambua picha na kuandika jina sahihi na wengine kufananisha na mnyama “kaa”. Wengine waliandika “mamba” na “kobe”. Majibu hayo siyo sahihi kwani kaa ana muonekano tofauti na chura. Aidha, mamba ni mrefu mnene ana magamba na kobe ni mnyama anayetembea na jumba lake.

Hata hivyo, wanafunzi 14,049 (47.86%) waliandika kwa usahihi jina “chura”. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutambua picha na kuhusianisha na jina sahihi linalowakilisha picha husika. Vilevile, uchambuzi ulibaini kuwa wanafunzi hao waliweza kubaini jina la picha hiyo kutokana na mnyama huyo kupatikana mara kwa mara katika maeneo wanayoishi.

(b) **Ua**

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 16,489 (56.17%) waliweza kuandika jina “ua” kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha umahiri wa kuhusianisha picha na jina kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha ya kutambua picha na wanafahamu maua katika mazingira yao ya kila siku. Vilevile, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuandika maneno yenye silabi zilizoundwa na irabu pekee. Silabi zinazoundwa na irabu pekee kimatamshi na kiuandishi ni rahisi kuliko silabi zinazoundwa na konsonanti na irabu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 12,867 (43.83%) walishindwa kuandika jina “ua” kwa usahihi na wengine kutoandika neno lolote. Baadhi yao waliandika majina yasiyohusiana na picha hiyo kama vile “uyoga” na “mawingu” majibu ambayo hayana uhusiano wowote na picha ya ua. Wengine waliandika neno “*uwa”* kwa kuongeza kiyeyusho “w” ili kurahisisha matamshi. Waliongeza sauti “w” kwa kuwa katika kutamka neno/maneno yanayoundwa kwa mfuatano wa irabu, kiyeyusho huongezwa kurahisisha matamshi lakini katika maandishi kiyeyusho hudondoshwa.

(c) **Mguu**

Uchambuzi zaidi wa utendaji wa wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 14,768 (50.31%)

walishindwa kuandika jina “mguu” kwa usahihi kwa sababu walikosa maarifa ya kulinganisha picha husika na jina. Baadhi yao waliandika jina kwa kutumia lugha ya asili kama vile, “muguu”, “mgulu”, “mnguu”, “miguu”, “muguhu” na wengine walitaja majina ambayo hayahusiani na picha husika ili hali wengine hawakuandika chochote.

Aidha, wanafunzi 14,588 (49.69%) waliweza kutambua picha na kuandika jina kwa usahihi. Wanafunzi hao waliweza kuunganisha konsonanti mbili “mg” na irabu mbili “uu” kisha kuunda neno mguu.

(d) **Meza**

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 21,686 (73.87%) waliweza kuandika jina “meza” kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutambua picha kwa sababu ni aina ya samani zinazopatikana katika mazingira mbalimbali kama vile shuleni, nyumbani na hospitalini.

Aidha, wanafunzi 7,670 (26.13%) hawakuwa na umahiri wa kuandika jina “meza” kikamilifu. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika maneno “mesa”, “imesa” “metha”, hii inatokana na kuathiriwa na lugha za asili katika maeneo wanayoishi. Vilevile, walishindwa kutofautisha sauti “s”, “z”, na “th”, kutokana na matamshi ya sauti hizo kuwa na sifa moja ya utamkwaji ambayo ni vikwamizi, na wengine hawakuandika kitu chochote.

(e) **Mpira**

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 16,811 (57.27% ) hawakuwa na umahiri wa kuandika jina “mpira” ambapo miongoni mwao waliandika “mpila”. Wanafunzi hao walishindwa kutofautisha sauti ya herufi “r” na “l”. Wengine waliandika “mupila” kwa sababu ya kuathiriwa na matamshi ya lugha za asili na hivyo kuongeza herufi “u” kwenye silabi “m”. Pia,

wapo walioandika maneno “boli”, “gozi”, “tufe” na “kitenesi”. Wanafunzi hawa walitambua picha ila waliandika maneno yasiyo sahihi kwa sababu katika muktadha wa mazingira yao hutumia maneno hayo kumaanisha mpira ambapo si Kiswahili sanifu.

Hata hivyo, wanafunzi 12,545 (42.73%) waliweza kutambua picha husika na kuandika neno “mpira”. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kuhusianisha picha husika na jina la picha lengwa kwa kuwa mpira hupatikana katika mazingira yanayowazunguka, hivyo ilikuwa rahisi kwa wanafunzi kutaja jina sahihi la picha husika.

(f) **Saa**

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 22,351 (76.14%) walikuwa na utendaji mzuri kwani waliweza kutambua picha husika na kuandika jina kwa usahihi “saa”. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuhusisha picha na kuunda herufi/silabi zinazounda neno “saa”. Aidha, neno hilo ni rahisi kwa kuwa limeandikwa kwa silabi ambazo ni konsonanti na irabu na irabu pekee.

Aidha, jumla ya wanafunzi 7,005 (23.86%) hawakuweza kuandika neno “saa” kwa usahihi kwa kuwa hawakuwa na umahiri wa kuunda herufi za neno “saa”. Hivyo, waliandika maneno yasiyo sahihi kama “sa”, “zaa” “thaa” na “saha”. Wanafunzi hao walishindwa kuandika kwa usahihi neno saa kwa sababu neno lina silabi mbili {sa} na {a}. Silabi ya kwanza imeundwa na konsonanti + irabu na silabi ya pili imeundwa na irabu pekee, hivyo ni rahisi kwa mwanafunzi kudondosha herufi “a” iliyosimama kama silabi ya pili ya neno “saa” na kuandika “*sa”.* Aidha, wanafunzi walioandika “saha” badala ya “saa” wameathiriwa na matamshi ya lugha za asili hivyo kuandika neno hilo kama wanavyotamka katika lugha husika.

(g) **Bata**

Jumla ya wanafunzi 19,791 (67.42%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina “bata”. Wanafunzi hao waliweza kuitambua picha waliyopewa na kuandika jina la picha hiyo kwa usahihi. Jina hilo linatumika sana katika mazingira ya maisha ya kawaida hivyo, walijua kuliandika kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 9,565 (32.58%) hawakuandika jina kwa usahihi kwa sababu hawakuwa na umahiri wa kuhusianisha picha na jina husika. Baadhi yao waliandika neno “samaki” kwa sababu picha hiyo (bata) ipo kwenye maji. Wengine walishindwa kuunganisha herufi na kuandika maneno yasiyohusiana na picha hiyo, kama vile, neno “bana” na kupata utendaji hafifu.

(h) **Ng’ombe**

Wanafunzi 18,374 (62.59%) walikuwa na utendaji hafifu katika kuunda maneno yenye ving’ong’o “ng’” (sauti za nazali) ambazo wakati wa utamkaji hewa hupitia kwenye chemba ya pua kutokea kinywani. Wanafunzi hao waliandika neno “ngombe” kwa kushindwa kuweka alama (’) katikati ya herufi “g” na “o” (ng’o). Aidha, wanafunzi wengine waliathiriwa na matamshi ya lugha ya asili hivyo kuandika jina lisilo sahihi kama vile “mang’ombe”.

Pamoja na uwepo wa utendaji hafifu kwa wanafunzi wengi, wanafunzi 10,982 (37.41%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "ng’ombe". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha husika na kuhusianisha na herufi za neno kisha kuandika kwa usahihi. Uchambuzi unaonesha kwamba, wanafunzi hawa walikuwa na umahiri mzuri katika kuunda maneno yenye sauti za ving’ong’o (ng’) kwa kuweka alama (’).

(i) **Jani**

Uchambuzi wa upimaji unaonesha kuwa wanafunzi 14,965 (50.98%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "jani". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha husika na kisha kuandika jina linalohusiana na picha hiyo kwa usahihi.

Aidha, wanafunzi 14,391 (49.02%) hawakuwa na umahiri mzuri katika kutambua jina linalohusiana na picha hiyo. Wanafunzi hao waliandika majina kama vile "ua", "tawi", "nanasi", "unyoya wa kuku" na "mti". Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kutosha wa kutambua picha waliyopewa ambapo walishindwa kutofautisha "jani" na "tawi" ingawa zote ni sehemu za mti. Wengine hawakuandika neno lolote.

(j) **Kikombe**

Wanafunzi 18,937 (64.51%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina lililowakilishwa na picha husika kwa sababu waliweza kuandika jina "kikombe". Wanafunzi hao walikuwa na umahiri mzuri wa kuunda konsonanti mwambatano "mb". Hii iliwawezesha kuandika kwa usahihi jina la picha lenye konsonanti mwambatano ambalo ni "kikombe".


Aidha, wanafunzi 10,419 (35.49%) hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuandika jina "kikombe". Wanafunzi hao waliandika majina kama vile *ikikobe, kikobe kkapiabe.* Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika *ikikombe*, *umunego* kutokana na athari za lugha za makabila. Aidha, wengine walishindwa kutokana na kukosa umahiri wa kuunda konsonanti mwambatano "mb".

### 3.4.2 Swali la 2: Kupigia Mstari Maneno Yaliyoandikwa kwa Herufi Ndogo

Katika swali la pili, wanafunzi walitakiwa kubaini na kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo katika makundi ya

maneno waliyopewa. Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutambua herufi kubwa na ndogo.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 28,816. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri. Wanafunzi 10,948 sawa na asilimia 37.29 walipigia mstari maneno 9 hadi 10 yaliyoandikwa kwa herufi ndogo, jambo linaonesha kuwa walikuwa na utendaji mzuri sana. Aidha, wanafunzi 3,637 sawa na asilimia 12.39 walikuwa na utendaji mzuri kwa kuweza kupigia mstari maneno 6 hadi 8. Wanafunzi 2,291 sawa na asilimia 7.80 walipata utendaji wa wastani kuanzia maneno 3 hadi 5. Vilevile, wanafunzi 12,480 sawa na asilimia 42.51 walipata utendaji hafifu kwa kupigia mstari maneno 0 hadi 2. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na. 7:** *Utendaji wa wanafunzi katika kutambua maneno yenye herufi ndogo.*

Uchambuzi wa upimaji unaonesha kuwa wanafunzi 12,480 (42.51%) walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kubainisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo. Miongoni mwao, walikuwepo wanafunzi waliopigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa, wengine waliandika neno moja linalowakilisha maneno yote kwenye kundi la maneno badala ya kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo. Aidha, wanafunzi wengine waliandika maneno hayo na kisha kupigia mstari. Wengine walipigia mstari maneno yote yaliyoorodheshwa. Kielelezo Na. 15 (a - c) ni sampuli za majibu ya wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu.

2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa **herufi ndogo**.

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi
(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu
(c) dawati, KITI, meza, KABATI
(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi
(e) fisi, MBUZI, twiga, SUNGURA

**Kielelezo Na. 15 (a):** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepigia mstari maneno yote.

2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa **herufi ndogo**.

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi
(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu
(c) dawati, KITI, meza, KABATI
(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi
(e) fisi, MBUZI, twiga. SUNGURA

**Kielelezo Na. 15 (b):** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.


2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa **herufi ndogo**

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi watu
(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu viungo
(c) dawati, KITI, meza, KABATI samani
(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi matunda
(e) fisi, MBUZI, twiga, SUNGURA wanyama

**Kielelezo Na. 15 (c):** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika jina moja linalowakilisha maneno yote katika makundi ya maneno kwa kila kipengele cha swali.

Kielelezo Na. 15 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu kinyume na matakwa ya swali, kwa kupigia mstari maneno yote na maneno yenye herufi kubwa. Aidha, kielelezo Na. 15 (c) kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeandika maneno jumuishi badala ya kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 2,291 (7.80%) walikuwa na utendaji wa wastani. Wanafunzi hao waliweza kupigia mstari baadhi ya maneno na kushindwa kupigia mstari maneno mengine. Miongoni mwao, wapo waliopigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na wengine walipigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na ndogo. Kielelezo Na. 16 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.




2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo.

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi
(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu
(c) dawati, KITI, meza, KABATI
(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi
(e) fisi, MBUZI, twiga, SUNGURA

**Kielelezo Na. 16:** Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.

Kielelezo Na.16 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani kwani aliweza kupigia mstari maneno matano (5) kwa usahihi kati ya maneno 10.

Aidha, asilimia 12.39 ya wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri. Wanafunzi hao waliweza kubaini maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo na kupiga mstari maneno hayo na kushindwa kupigia mstari maneno mengine. Kielelezo Na. 17 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.



2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi
(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu
(c) dawati, KITI, meza, KABATI
(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi
(e) fisi, MBUZI, twiga, SUNGURA

**Kielelezo Na. 17:** sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.

Kielelezo Na.17 kinaonesha mwanafunzi aliyeweza kupigia mstari maneno 6 kati ya maneno 10 yaliyoandikwa kwa herufi ndogo hivyo kuonyesha utendaji mzuri.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 10,948 (37.29%) walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi hao waliweza kubaini na kupigia mstari maneno yote yaliyoandikwa kwa herufi ndogo kwa usahihi katika vipengele vyote. Kielelezo Na. 18 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.

2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa **herufi ndogo**.

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi

(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu

(c) dawati, KITI, meza, KABATI

(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi

(e) fisi, MBUZI, twiga, SUNGURA

**Kielelezo Na.18**: sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.


Katika Kielelezo Na.18, mwanafunzi aliweza kupigia mstari maneno 10 yenye herufi ndogo kwa usahihi na kuwa na utendaji mzuri sana.

### 3.4.3 Swali la 3: Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi

Swali lilikuwa na alama 20 na lilipima umahiri wa mwanafunzi kunakili maneno na kuweka alama za uandishi ambazo ni; nukta (.), mkato (,), kushangaa (!) na kuuliza (?) katika nafasi zilizoachwa wazi kwenye kifungu cha maneno.


Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 28,816 (100%). Kiwango cha utendaji kwa ujumla katika swali hili kilikuwa kizuri. Uchambuzi unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 9,518 sawa na asilimia 32.42 walikuwa na utendaji mzuri sana ambapo walipata alama kuanzia 16 hadi 20. Wanafunzi hawa waliweza kunakili maneno yote na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Aidha, wanafunzi 6,944 sawa na asilimia 23.65 walikuwa na utendaji mzuri kwa kuweza

kunakili baadhi ya maneno na kutumia baadhi ya alama za uandishi kwa usahihi na kupata alama kuanzia 11 hadi 15. Wanafunzi 1,912 sawa na asilimia 6.51 walikuwa na utendaji wa wastani ambapo walipata alama kuanzia 6 hadi 10. Vilevile, wanafunzi 10,982 sawa na asilimia 37.41 walikuwa na utendaji hafifu kwani walipata alama kuanzia 0 hadi 5 kwa kuwa walishindwa kunakili maneno kutoka kwenye kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. Chati Na. 8 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 8**: *Utendaji wa wanafunzi katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi.*

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 10,982 (37.41%) walikuwa na utendaji hafifu kwani walishindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Miongoni mwao wapo walioandika maneno yasiyoeleweka na wengine walioandika herufi zinazounda maneno yasiyo na maana yoyote katika lugha ya Kiswahili. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kunakili maneno kutoka katika swali la 2. Kielelezo Na. 19 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi hao.


3. **Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!), na alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.


Umeiona ile bustani yenye maua mazuri ___ Looh ___ inapendeza sana ___ pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi ___

Pigja mstari maneno yaliyoandikwakwa herusindogo
(a) MVULANA msiChana BABUbibi
(b) NYANYA KAROTIpilipili Kitunguu
(c) dawati KITImeza KABATI
(d) PAPAI peraNANYAsi fenesi
(e) fisiMBUZItuga SUNGUA

**Kielelezo Na.19**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi.

Kielelezo Na.19 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na umahiri hafifu ambapo alinakili swali la pili badala ya kunakili kifungu cha maneno kisha kuweka alama za uandishi kwa usahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 1,912 (6.51%) walikuwa na utendaji wa wastani kwani waliweza kunakili baadhi ya maneno waliyopewa. Baadhi yao waliweka alama za uandishi mahali ambapo siyo sahihi na wengine walishindwa kuunda herufi za maneno waliyopaswa kunakili. Wanafunzi hao hawakuwa na Stadi ya Kuandika na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi sahihi ya alama za uandishi. Kielelezo Na. 20 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani katika swali la 3.




3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!), na alama ya kuuliza (?) mahali panapostahili.

Umeiona ile bustani yenye maua mazuri ___ Looh ___ inapendeza sana ___ pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi ___

**Kielelezo Na. 20**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji wa wastani.

Kielelezo Na. 20 Kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyenakili baadhi ya maneno kwa usahihi na kushindwa kuweka alama za uandishi.

Vilevile, wanafunzi 6,944 (23.65%) walikuwa na utendaji mzuri kwa kuwa walikuwa na stadi ya kuunda baadhi ya maneno kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuandika maneno kwani waliweza kunakili baadhi ya maneno kutoka katika kifungu cha maneno kwa usahihi. Aidha, miongoni mwao wapo walioweka baadhi ya alama za uandishi mahali pasipo sahihi na wengine ambao hawakuweka kabisa. Kielelezo Na. 21 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri katika swali la 3.



3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)**, na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.


Umeiona ile bustani yenye maua mazuri (?) Looh ? inapendeza sana . pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi !

Umeiona ile bustani yenye maua mazuri inapendeza sana pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi

**Kielelezo Na. 21:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri.

Kielelezo Na.21 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyenakili baadhi ya maneno kwa usahihi, hata hivyo alishindwa kujaza alama za uandishi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 9,518 (32.42%) walikuwa na utendaji mzuri sana kwani waliweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. Kielelezo Na. 22 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.



3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)**, na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Umeiona ile bustani yenye maua mazuri ____ Looh ____ inapendeza sana ____ pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi ____

Umeiona ile bustani yenye maua mazuri ? Looh! inapendeza sana, pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi.

**Kielelezo Na. 22:** Majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana.


Kielelezo Na.22 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekuwa na utendaji mzuri sana kwani alinakili kifungu cha maneno na kuweka alama zote za uandishi kwa usahihi.

## 3.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Mikoa, Mahali Shule Ilipo (Mijini/Vijijini) na Jinsi (Wavulana/Wasichana).

Ulinganifu ulifanyika kwa lengo la kubainisha utendaji wa wanafunzi kimkoa, mahali shule ilipo (mjini au kijijini) na jinsi. Vilevile, ulinganifu huo ulifanyika ili kubainisha changamoto zilizopo na kutoa mapendekezo ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi ya Kuandika.

### 3.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa

Katika upimaji wa stadi ya kuandika, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kimikoa kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 9.





**Chati Na. 9**: *Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Kimikoa.*

Chati Na. 9 inaonesha asilimia ya utendaji wa wanafunzi Kimikoa. Uchambuzi unaonesha kuwa katika baadhi ya Mikoa wanafunzi walikuwa na kiwango kizuri cha utendaji ukilinganisha na Mikoa mingine. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na utendaji wa kiwango cha wastani hadi mzuri sana (95.2%), ukifuatiwa na mkoa wa Morogoro (93.6%) na Njombe (88.1%).

Kwa upande mwingine, mkoa wa Kigoma ulikuwa na kiwango cha chini cha utendaji kuanzia wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 51.9, ukifuatiwa na mkoa wa Katavi (60.1%) na mkoa wa Mwanza (63.9%). Mikoa mingine ilikuwa na utendaji kama inavyoonekana kwenye chati namba 9.

### 3.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa Kuzingatia Mahali Shule Zilipo

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 28,816 walifanya upimaji kwa mwaka 2019. Miongoni mwao, wanafunzi 10,269 walitoka shule za mijini na wanafunzi 19,087 walitoka shule za vijijini. Ulinganifu wa utendaji ulibaini kuwa kulikuwa na tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wa mijini na vijijini kwa kuwa Shule za mijini zina miundombinu ya kutosha pamoja na walimu wengi. Aidha, Shule za vijijini zina upungufu wa miundombinu pamoja na upungufu wa walimu. Chati Na. 10 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi wa shule za mijini na vijijini.





**Chati Na. 10**: *Ulinganifu wa Utendaji wa wanafunzi kwa shule za mjini na vijijini.*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa asilimia 80.3 ya utendaji wa wanafunzi kutoka shule za mjini ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana ikilinganishwa na utendaji wa shule za vijijini ambapo walikuwa na asilimia 72.5.

### 3.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa kuzingatia Jinsi

Uchambuzi wa upimaji unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 28,816 walifanya upimaji katika stadi ya Kuandika mwaka 2019. Kati yao, wavulana walikuwa 14,315 na wasichana 15,041.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wasichana walikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganishwa na wavulana. Chati Na. 11 inaonesha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia jinsi.




**Chati Na. 11**: *Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia Jinsi.*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi ambapo wasichana walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 77.20 na wavulana walikuwa na utendaji wa asilimia 73.00. Kwa ujumla, wasichana walifanya vizuri zaidi ya wavulana kwa tofauti ya asilimia 4.31. Aidha, wavulana walikuwa na utendaji hafifu kwa asilimia 27.00 wakati wasichana walikuwa asilimia 22.70.

## 3.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuandika

Uchambuzi wa Stadi ya Kuandika unaonesha kuwa wanafunzi 21,670 (75.20%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha ulikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganisha na umahiri wa kubainisha herufi ndogo na kunakili kifungu cha maneno pamoja na kuweka alama za uandishi.

Wanafunzi 22,844 (77.82%) walikuwa na umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa kuwa waliweza kuandika majina sahihi ya picha 3 hadi 10. Aidha, wanafunzi 18,374 (62.59%) walikuwa na umahiri

wa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. Wanafunzi hao walinakili maneno 6 hadi 16 ya kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi 1 hadi 4 kwa usahihi.

Vilevile, wanafunzi 16,876 (57.49%) walikuwa na umahiri wa kubainisha herufi ndogo. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana wa kutambua herufi ndogo kwa kuwa waliweza kupigia mstari maneno 3 hadi 10 kwa usahihi.

# SURA YA NNE

## UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu uliofanyika kwa kubainisha muundo wa karatasi ya upimaji ya mwaka 2020, vigezo vya kupima umahiri wa wanafunzi na uchambuzi wa takwimu na majibu ya wanafunzi. Aidha, sura hii inaeleza maeneo ambayo wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri sana, mzuri, wastani na hafifu. Pia, katika uchambuzi huo, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia maeneo mbalimbali. Maeneo hayo ni jinsi, mahali shule ilipo (mijini/vijijini) na mikoa. Aidha, sura hii imehitimishwa kwa muhtasari wa uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji katika Stadi ya Kuhesabu.

### 4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji

Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu ulikuwa na karatasi mbili na kila karatasi ilikuwa na maswali 10. Karatasi ya kwanza ilipima uwezo wa wanafunzi katika kutambua namba zinazokosekana kwenye mfululizo wa namba na kufumbua mafumbo. Katika karatasi hiyo, wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kwa kuandika majibu kwenye nafasi zilizoachwa wazi. Aidha, karatasi ya pili ilipima umahiri wa wanafunzi katika kujumlisha na kutoa namba nzima ambapo wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kwa mdomo. Majibu ya wanafunzi yaliandikwa na msimamizi wa upimaji kwenye fomu maalum (skeli ya upimaji) ya kujaza alama za wanafunzi au kudakwa moja kwa moja kwenye mfumo maalum wa kutunza kumbukumbu kwa kutumia kishikwambi (*tablet)*.

Karatasi zote mbili ziliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi za serikali ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili kufundishia. Karatasi ya kwanza ilikuwa na jumla ya alama thelathini ambapo kila swali katika umahiri wa kutambua namba zinazokosekana katika mfululizo lilikuwa na alama mbili na kila swali kwenye umahiri wa kufumbua mafumbo lilikuwa na alama nne. Karatasi ya pili ilikuwa na jumla ya alama ishirini ambapo kila swali lilikuwa na alama mbili. Hivyo, karatasi zote mbili zilikuwa na jumla ya alama hamsini.

## 4.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuhesabu

Katika upimaji wa Stadi ya Kuhesabu, kigezo cha utendaji wa mwanafunzi kilichotumika kwa kila umahiri kimegawanyika katika viwango vinne ambavyo ni: utendaji hafifu kwa mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hata moja au aliyejibu kwa usahihi swali moja au mawili; utendaji wa wastani kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali matatu; utendaji mzuri kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali manne; na utendaji mzuri sana kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano.

## 4.4 Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu

Takwimu zinaonesha kuwa wanafunzi 28,022 walifanya upimaji wa umahiri wa kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba na kufumbua mafumbo wakati wanafunzi 28,816 walipimwa umahiri wa kujumlisha na kutoa namba katika Stadi ya Kuhesabu. Hata hivyo, wanafunzi 794 sawa na asilimia 2.76 hawakufanya upimaji wa kutambua namba na kufumbua mafumbo lakini walifanya upimaji wa kujumlisha na kutoa. Idadi na asilimia ya wanafunzi wenye utendaji hafifu, wastani, mzuri na mzuri sana kwa kila umahiri uliopimwa imeoneshwa katika Jedwali Na.5.

**Jedwali Na.5: Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu**

| Umahiri Uliopimwa | Utendaji wa Wanafunzi | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu | | Wastani | | Mzuri | | Mzuri Sana | |
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Kutambua Namba zinazokosekana | 18,243 | 62.06 | 4,729 | 16.09 | 2,716 | 9.24 | 3,707 | 12.61 |
| Kujumlisha | 16,665 | 57.83 | 5059 | 17.56 | 3,412 | 11.84 | 3,681 | 12.77 |
| Kutoa | 19,144 | 66.43 | 4432 | 15.38 | 2,724 | 9.45 | 2,517 | 8.73 |
| Kufumbua Mafumbo | 19,001 | 64.64 | 4,359 | 14.83 | 3,400 | 11.57 | 2,635 | 8.96 |

Jedwali Na.5 linaonesha kuwa asilimia 62.06, 57.83, 66.43 na 64.64 ya wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi maswali matatu hadi matano katika kutambua namba zinazokosekana, kujumlisha, kutoa na kufumbua

mafumbo, mtawalia. Kwa ujumla wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri katika umahiri wa Kujumlisha na utendaji hafifu katika umahiri wa Kutoa.


Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na wastani wa alama 4.11 katika umahiri wa kutafuta namba inayokosekana kwenye mfululizo, jambo linalomaanisha kuwa walikuwa na uwezo wa kujibu maswali mawili hadi matatu kati ya matano. Aidha, katika maswali ya kufumbua mafumbo, walikuwa na wastani wa alama 7.71 ikimaanisha kuwa walikuwa na uwezo wa kujibu kwa usahihi swali moja hadi mawili kati ya matano. Katika maswali ya Kujumlisha na Kutoa, wanafunzi walipata wastani wa alama 7.88, jambo linalomaanisha kuwa walikuwa na uwezo wa kujibu kwa usahihi maswali matatu hadi manne kati ya kumi. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na wastani wa alama 19.76 kati ya 50 ambao ni utendaji wa wastani.

## 4.5 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanyika kwa kila swali ili kubaini utendaji wao katika kila umahiri.

### 4.5.1 Umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mfululizo wa Namba

Umahiri wa wanafunzi wa kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba ulipimwa katika swali la 1 hadi 5. Maswali hayo yalipima uwezo wa wanafunzi wa kutambua namba zinazokosekana na kuandika majibu kwenye nafasi zilizoachwa wazi. Katika swali la 1, 3, 4 na 5 kulikuwa na mfululizo wa namba zinazoongezeka wakati katika swali la 2 ulitolewa mfululizo wa namba zinazopungua. Chati Na. 12 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 1 hadi 5.




**Chati Na. 12:** *Asilimia ya wanafunzi walioweza kutambua namba inayokosekana kwenye mfululizo wa namba katika kila swali.*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa wanafunzi walikuwa na uwezo mkubwa wa kujibu kwa usahihi swali la 1, 4 na 2 ikilinganishwa na swali la 3 na 5 katika umahiri huu. Hii inaonesha kwamba wanafunzi hao walikuwa na umahiri mzuri zaidi katika kubaini namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba zinazotofautiana kwa 1 au 10 kuliko mfululizo wa namba zinazotofautiana kwa 2 au 5. Zaidi ya hayo, wanafunzi walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwenye mfululizo wa namba zinazopungua.

Aidha, Chati Na. 12 inaonesha kuwa wanafunzi 20,436 (69.52%) waliweza kujibu swali la 1 kwa usahihi katika upimaji ikilinganishwa na maswali mengine. Hivyo, wanafunzi walikuwa na kiwango kizuri zaidi cha kufaulu katika swali hili. Hata hivyo, wanafunzi wachache (20.65%) walijibu swali la 3 kwa usahihi. Hivyo, swali hili lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha kufaulu katika dhana ya kubaini namba zinazokosekana kwenye mfululizo wa namba zinazoongezeka kwa 2.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 11,152 sawa na asilimia 37.94 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika kubaini namba inayokosekana katika mfululizo

wa namba kama inavyoonekana katika Jedwali Na.5. Hii inaonesha kuwa walikuwa na uelewa mzuri katika dhana ya mpangilio wa namba. Kielelezo Na. 23 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano.

Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 3, 4, 5, 6, 7, 8.
2. 27, 26, 25, 24, 23.
3. 54, 56, 58, 60, 62.
4. 10, 20, 30, 40, 50.
5. 40, 45, 50, 55, 60.

**Kielelezo Na. 23**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi namba zinazokosekana katika maswali yote.

Kielelezo Na. 23 kinaonesha kuwa mwanafunzi aliweza kutambua tendo la kihisabati lililotumika ili kupata namba inayokosekana katika kila mfululizo. Mwanafunzi huyo alitambua kuwa, katika swali la 1, 3, 4 na 5, namba zinazoongezeka kwa 1, 2, 10 na 5, mtawalia. Aidha, katika swali la 2, mwanafunzi alitambua kuwa namba zilizopo kwenye mfululizo uliotolewa zinapungua kwa 1.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 4,731 sawa na asilimia 16.08 walikuwa na utendaji wa wastani. Wanafunzi hao waliweza kujibu maswali matatu kati ya matano kwa usahihi. Majibu yao yanaonesha kuwa walishindwa kutumia kanuni sahihi za kubaini namba zinazokosekana katika mifululizo iliyotolewa kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 24.

Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 3, 4, 5, 6 , 7, 8.
2. 27, 26, 25, 24, 23 .
3. 54, 56, 58, [illegible], 62.
4. 10, 20 , 30, 40, 50.
5. 40, 45, [illegible], 55, 60.

**Kielelezo Na. 24**: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi swali la 1, 2 na 4.

Katika Kielelezo Na. 24, mwanafunzi alishindwa kubaini kuwa katika swali la 3 na 5 namba zinaongezeka kwa 2 na 5 mtawalia.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 18,255 sawa na asilimia 62.06 walikuwa na utendaji hafifu kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.5. Baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya maswali hivyo hawakuandika majibu. Wengine waliandika majibu ambayo hayana uhusiano na mfululizo wa namba uliotolewa kwa kuwa, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya namba zinazokosekana kwenye mfululizo. Kielelezo Na. 25 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali moja tu kati ya maswali matano yaliyoulizwa.

Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 3, 4, 5, 6 , 7, 8.
2. 27, 26, 25, 24, [illegible].
3. 54, 56, 58, [illegible] , 62.
4. 10, [illegible], 30, 40, 50.
5. 40, 45, [illegible], 55, 60.

**Kielelezo Na. 25:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu swali 1 tu.

Katika Kielelezo Na. 25, mwanafunzi aliongeza 1 kwenye namba iliyotangulia katika maswali yote manne bila kuzingatia tofauti iliyopo kati ya namba zinazofuatana. Pia, aliongeza 1 kwenye

namba 24 na kupata 25 katika swali la 2 kwa kudhani kuwa mfululizo uliotolewa ni wa namba zinazoongezeka. Mwanafunzi huyo alipaswa kutoa 1 kutoka katika namba 24 ili kupata namba inayofuata. Hii inatokana na ukweli kwamba mfululizo huo unahusisha namba zinazopungua kwa 1.

### 4.5.2 Umahiri wa Wanafunzi katika Kujumlisha

Katika maswali ya umahiri wa Kujumlisha, wanafunzi walitakiwa kujibu kwa mdomo. Karatasi hiyo ilikuwa na maswali kumi ambapo matano yalikuwa ya kujumlisha kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na.6**: **Maswali ya Kujumlisha**

| Namba ya swali | Swali |
|---|---|
| 1 | 11 + 6 = ☐ |
| 2 | 15 + 8 = ☐ |
| 3 | 11 + 23 = ☐ |
| 4 | 27 + 36 = ☐ |
| 5 | 42 + 18 = ☐ |


Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa;

(a) swali la 1 na 3 yalipima uwezo wa wanafunzi katika kujumlisha namba bila kubeba. Swali la 1 lilihusu kujumlisha namba yenye tarakimu mbili na namba nyingine yenye tarakimu moja. Aidha, swali la 3 lilihusu kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja.

(b) swali la 2, 4 na 5 yalipima uwezo wa wanafunzi katika kujumlisha namba kwa kubeba. Katika swali la 2, mwanafunzi alitakiwa kujumlisha namba moja yenye tarakimu mbili na namba nyingine yenye tarakimu moja. Swali la 4 na 5 yalihusu kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja.

Katika upimaji huo, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi maswali manne ya mwanzo ya kujumlisha hawakuendelea na

swali la tano, badala yake walielekezwa kujibu maswali ya kutoa. Vile vile, wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi maswali manne ya mwanzo ya kutoa hawakuruhusiwa kuendelea na swali la tano. Chati Na. 13 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika maswali ya kujumlisha (swali la 1 hadi 5).




**Chati Na. 13**: *Asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali ya kujumlisha namba.*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa asilimia 64.69 na 53.5 ya wanafunzi walikuwa na uwezo mzuri zaidi katika kujibu swali la 1 na 2 mtawalia, ikilinganishwa na maswali mengine. Hata hivyo, wanafunzi walikuwa na utendaji wa chini katika swali la 4 (23.58%) na 5 (26.43%) kwa sababu maswali haya yalihitaji kubeba wakati wa kujumlisha.

Pamoja na utendaji mzuri ulioonеshwa, wanafunzi wachache (23.58% na 26.43%) kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 13, waliweza kujibu kwa usahihi maswali ya kujumlisha kwa kubeba (4 na 5) kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi yao hawakuongeza kwenye makumi namba walizobeba kutoka kwenye mamoja. Wengine walijumlisha mamoja pekee na hawakuendelea ili kupata jibu lililotakiwa. Aidha, wanafunzi wengine walishindwa kujibu maswali kutokana na kutokuwa na

uwezo wa kusoma na kuandika. Kwa mfano, katika swali la 4, baadhi ya wanafunzi walijibu kwa mdomo kuwa jibu ni 53 badala ya 63. Katika swali la 2, wanafunzi wengine walijumlisha 8 na 1 na kupata 95 badala ya kujumlisha 8 na 5 ikifuatiwa na makumi ili kupata 23.

### 4.5.3 Umahiri wa Wanafunzi katika Kutoa

Umahiri wa wanafunzi katika kutoa namba ulihusisha swali la 6 hadi la 10 kama inavyoonekana katika jedwali Na. 7:

**Jedwali Na.7: Maswali ya Kutoa**


| Namba ya Swali | Swali |
|---|---|
| 6 | 17 - 3 = ☐ |
| 7 | 20 - 8 = ☐ |
| 8 | 35 - 24 = ☐ |
| 9 | 46 - 19 = ☐ |
| 10 | 50 - 21 = ☐ |

Jedwali Na.7 linaonesha kuwa;

(a) swali la 6 na 8 yalipima uwezo wa wanafunzi katika kutoa bila kukopa. Swali la 6 lilihusu kutoa namba yenye tarakimu moja kutoka kwenye namba yenye tarakimu mbili. Aidha, swali la 8 lilikuwa na namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja.

(b) swali la 7, 9 na 10 yalipima uwezo wa wanafunzi katika kutoa kwa kukopa. Katika swali la 7, wanafunzi walitakiwa kutoa namba yenye tarakimu moja kutoka kwenye namba yenye tarakimu mbili kwa kukopa. Swali la 9 na 10 yalihusu kutoa namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja.

Chati Na.14 inaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa maswali ya kutoa namba.




**Chati Na. 14**: *Asilimia ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali ya kutoa namba.*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na utendaji mzuri katika swali la 6 (56.08%) na 7 (47.02%) ikilinganishwa na maswali mengine. Wanafunzi hao walifanya vizuri katika maswali hayo kwa kutumia zana za kuhesabia kama vile kuhesabu vidole. Hata hivyo, wanafunzi walikuwa na utendaji wa chini katika swali la 9 na 10 katika umahiri huu. Hii ni kwa sababu maswali haya yalihitaji kukopa wakati wa kutoa.

### 4.5.4 Umahiri wa Wanafunzi katika Kufumbua Mafumbo


Uwezo wa wanafunzi katika kufumbua mafumbo ulipimwa katika swali la 6 hadi 10 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na.8: Maswali ya Mafumbo**

| Namba ya Swali | Swali |
|---|---|
| 6 | Kikapu kina machungwa 3. Iwapo yataongezwa machungwa 2, kikapu hicho kitakuwa na |

| | |
|---|---|
| | machungwa mangapi? |
| 7 | Juma alikuwa na pipi 7. Alimpa rafiki yake pipi 4. Je, alibakiwa na pipi ngapi? |
| 8 | Daftari langu la kuandika lina kurasa 48. Ikiwa kurasa 32 zimejaa, je, zimebaki kurasa ngapi? |
| 9 | Musa alinunua mayai 33 siku ya kwanza. Siku ya pili alinunua mayai 19. Je, Jumla alinunua mayai mangapi? |
| 10 | Mwalimu alikuwa na penseli 51. Aliwapa wanafunzi penseli 17. Je, alibakiwa na penseli ngapi? |

Maswali hayo yalipima umahiri wa wanafunzi wa kufumbua mafumbo yanayohusiana na maisha ya kila siku kwa kutumia dhana ya kujumlisha au kutoa. Utendaji wa wanafunzi katika umahiri huu umeoneshwa kwenye Chati Na. 15.





**Chati Na. 15:** *Asilimia ya wanafunzi waliofumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa.*

Chati Na. 15 inaonesha kuwa swali la 6 lilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wanafunzi (62.0%) walioweza kufumbua kwa usahihi fumbo lililotolewa likifuatiwa na swali la 7 na 8. Kwa upande mwingine, idadi ya wanafunzi waliofumbua kwa usahihi fumbo lililotolewa katika swali la 10 ilikuwa ndogo zaidi (19.01%) katika umahiri wa kufumbua mafumbo.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa kati ya wanafunzi 28,022 waliopimwa katika umahiri wa kufumbua mafumbo, wanafunzi 5,994 sawa na asilimia 20.53 walikuwa na utendaji mzuri wakati wanafunzi 4,359 sawa na asilimia 14.83 walikuwa na utendaji wa wastani.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa baadhi ya wanafunzi waliofanya vizuri katika umahiri wa kufumbua mafumbo walikuwa na uwezo wa kutumia kwa usahihi matendo ya kujumlisha na kutoa. Hivyo, wanafunzi hao waliweza kufumbua mafumbo yaliyotolewa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 26.


6. Kikapu kina machungwa 3. Iwapo yataongezwa machungwa 2, kikapu hicho kitakuwa na machungwa mangapi?


3
+ 2
5

7. Juma alikuwa na pipi 7. Alimpa rafiki yake pipi 4. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

7
− 4
3

8. Daftari langu la Kuandika lina kurasa 48. Ikiwa kurasa 32 zimejaa, je, zimebaki kurasa ngapi ambazo hazijaandikwa?

48
− 32
16


9. Musa alinunua mayai 33 siku ya kwanza. Siku ya pili alinunua mayai 19. Je, jumla alinunua mayai mangapi?

  33
+ 19
  52


10. Mwalimu alikuwa na penseli 51. Aliwapa wanafunzi penseli 17. Je, alibakiwa na penseli ngapi?

  51
- 17
  34

**Kielelezo Na. 26:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefumbua kwa usahihi mafumbo yaliyotolewa.

Katika Kielelezo Na. 26, mwanafunzi aliweza kufumbua mafumbo yote yaliyotolewa kwa kutumia zana za kuhesabia na matendo ya kihisabati, hivyo kupata majibu sahihi katika maswali yote.

Wanafunzi wengine walijibu maswali yote kwa kuhesabu vidole, kutali au kutumia karatasi na penseli wakati wa kutafuta majibu. Kielelezo Na. 27 kinaonesha kazi ya mwanafunzi aliyeweza kufumbua kwa usahihi mafumbo yote.



6 Kikapu kina machungwa 3. Iwapo yataongezwa machungwa 2, kikapu hicho kitakuwa na machungwa mangapi?

= 5

7 Juma alikuwa na pipi 7. Alimpa rafiki yake pipi 4. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

=3.

8 Daftari langu la Kuandika lina kurasa 48. Ikiwa kurasa 32 zimejaa, je, zimebaki kurasa ngapi ambazo hazijaandikwa?

16

9. Musa alinunua mayai 33 siku ya kwanza. Siku ya p... alinunua mayai 19. Je, jumla alinunua mayai mangapi?

52

10. Mwalimu alikuwa na penseli 51. Aliwapa wanafu... penseli 17. Je, alibakiwa na penseli ngapi?

34

**Kielelezo Na. 27:** Sampuli ya kazi ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali ya mafumbo.

Katika Kielelezo Na. 27, mwanafunzi alichora viduara na kuvihesabu kwa kutali wakati wa kujumlisha na kutoa namba katika kufumbua mafumbo yaliyotolewa na hivyo, kupata majibu sahihi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 19,001 sawa na asilimia 64.64 walikuwa na utendaji hafifu kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5. Baadhi yao walishindwa kufumbua mafumbo yote yaliyotolewa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulibainisha kuwa sababu zilizowafanya kuwa na utendaji hafifu zinaweza kuwa kati ya hizi zifuatazo:

(a) Kukosa maarifa ya kutosha kuhusu kujumlisha na kutoa namba. Katika swali la 6, 7 na 8 baadhi ya wanafunzi walijumlisha badala ya kutoa namba zilizotolewa. Vile vile, katika swali la 9 wapo wanafunzi walioshindwa kujumlisha kwa kubeba. Kwa mfano, waliandika "33 + 19 = 412", "33 + 19 = 42" au "33 + 19 = 124" ambayo siyo majibu sahihi. Wengine waliandika "$51+17=44$" au "$51+17=46$" ambayo siyo majibu sahihi.

(b) Kushindwa kuelewa maana ya maneno kama vile "yataongezwa", "alibakiwa", "zimebaki" na "jumla", ambayo yalitumika katika mafumbo yaliyotolewa.

(c) Kunakili mafumbo yaliyotolewa badala ya kuyafumbua.

(d) Kutojibu maswali au kuandika majibu yasiyohusiana na mafumbo yaliyotolewa, jambo linalodhihirisha kuwa wanafunzi hawakujua kusoma na kuandika.


Kielelezo Na. 28 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi maswali yote matano katika umahiri huu.

6. Kikapu kina machungwa 3. Iwapo yataongezwa machungwa 2, kikapu hicho kitakuwa na machungwa mangapi?

3 − 2 = 1

7 Juma alikuwa na pipi 7 Alimpa rafiki yake pipi 4. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

[illegible]


8. Daftari langu la Kuandika lina kurasa 48. Ikiwa kurasa 32 zimejaa, je, zimebaki kurasa ngapi ambazo hazijaandikwa?

48 + 32 = 710

9. Musa alinunua mayai 33 siku ya kwanza. Siku ya pili alinunua mayai 19. Je, jumla alinunua mayai mangapi?

33 + 19 = 124

10. Mwalimu alikuwa na penseli 51. Aliwapa wanafunzi penseli 17. Je, alibakiwa na penseli ngapi?

51 − 17 = 26

**Kielelezo Na. 28:** Sampuli ya majibu mwanafunzi aliyeshindwa kufumbua mafumbo yote.


Katika kielelezo Na.28, mwanafunzi alitoa badala ya kujumlisha katika swali la 6, 7 na 8. Aidha, mwanafunzi huyo alikosa maarifa ya kujumlisha namba zenye tarakimu mbili katika swali la 9. Kwa mfano, alijumlisha mamoja akaandika jibu upande wa makumi bila kubeba, kisha akajumlisha makumi na kuyaandika upande wa mamoja. Pia, katika swali la 10, alishindwa kutoa namba zenye tarakimu mbili kwa kukopa.

## 4.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi

Ulingalifu wa utendaji wa wanafunzi waliopimwa katika stadi ya Kuhesabu umefanyika katika maeneo mawili ya uchambuzi. Eneo la kwanza ni ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia jinsi katika upimaji wa umahiri wa kubaini namba inayokosekana katika mfululizo wa namba na kufumbua mafumbo. Eneo la pili ni ulinganifu wa utendaji wao kwa jinsi katika upimaji wa umahiri wa kujumlisha na kutoa namba.

### 4.6.1 Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia Jinsi katika Upimaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo

Uchambuzi unaonesha kuwa jumla ya wanafunzi 28,022 walifanya Upimaji wa maswali ya kubaini namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba na kufumbua mafumbo, wanafunzi 15,046 walikuwa wavulana wakati 14,349 walikuwa wasichana. Chati Na. 16 inaonesha asilimia ya wavulana na wasichana waliojibu kwa usahihi.





**Chati Na.16**: *Matokeo ya jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa wavulana na wasichana.*

Chati Na. 16 inaonesha kuwa asilimia 39.10 ya wasichana walikuwa na utendaji wastani hadi mzuri sana katika umahiri wa kutambua namba katika mfululizo ikilinganishwa na asilimia 36.83 ya wavulana. Pia, Chati hii inaonesha kuwa wavulana na wasichana walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 37.98 na 32.62, mtawalia, katika umahiri wa kufumbua mafumbo. Hii inaonesha kuwa wavulana walikuwa na utendaji mzuri zaidi kuliko wasichana kwa kila umahiri.

### 4.6.2 Ulinganifu wa Jinsi katika Upimaji wa Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi 28,816 walipimwa kwa maswali ya umahiri wa kujumlisha na kutoa namba katika Stadi ya Kuhesabu. Katika umahiri huo, wanafunzi 14,010 walikuwa wavulana wakati 14,807 walikuwa wasichana. Chati Na. 17 inaonesha asilimia ya wavulana na wasichana waliojibu kwa usahihi maswali yaliyokuwa katika umahiri wa kujumlisha na kutoa namba.




**Chati Na. 17**: *Matokeo ya jumla kwa kuzingatia ulinganifu wa Jinsi.*

Chati Na. 17 inaonesha ulinganifu wa kiwango cha kufaulu cha wavulana na wasichana katika kila swali. Kwa mfano, katika maswali ya kutoa, wavulana waliojibu kwa mdomo swali ambalo liliuliza “50-21=” kwa usahihi ni asilimia 19.18 wakati wasichana ni asilimia 19.32. Hata hivyo, tofauti kati ya wavulana na wasichana kwa viwango vyote vya utendaji ilikuwa


ndogo. Wavulana na wasichana walifanya vizuri katika swali la 1 na 6 ikilinganishwa na maswali mengine.

## 4.7 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi unalenga kubaini maeneo ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele zaidi kuliko mengine ili serikali, taasisi na wadau mbalimbali waweze kuchukua hatua za kuboresha utendaji wa stadi ya Kuhesabu katika maeneo hayo. Kwa sababu hiyo, matokeo ya wanafunzi yamelinganishwa kwa kuzingatia shule za kijijini na shule za mjini. Aidha, uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi umefanyika kwa kuhusisha mikoa yote ya Tanzania Bara.

### 4.7.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini

Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu wa maswali ya kujibu kwa kuandika ulihusisha wanafunzi 10,285 kutoka shule za mijini na 19,110 kutoka shule za vijijini. Ulinganifu wa utendaji umefanyika ili kubaini kama kuna tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wa mijini na vijijini. Matokeo ya ulinganifu huu yameoneshwa katika Chati Na. 18.





**Chati Na.18**: *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa shule za mijini na vijijini.*

Chati Na. 18 inaonesha kuwa katika kila kiwango kuna tofauti ya utendaji wa wanafunzi wa shule za vijijini ikilinganishwa na mijini. Aidha, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa shule za mijini ni asilimia 68.44 na kwa shule za vijijini ni asilimia 61.50. Hii inaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi wa shule za mijini ni mzuri zaidi ikilinganishwa na shule za vijijini.

### 4.7.2 Ulinganifu wa Utendaji katika Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa Namba kwa Kuzingatia Shule za Mijini na Vijijini

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika maswali ya kujumlisha na kutoa ulifanyika ili kubaini tofauti katika utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatika maeneo shule zilipo. Ulinganifu huu ulifanyika ili kubaini kama utendaji wao unaonesha mahitaji ya jitihada zaidi za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo ya ulinganifu huo yameoneshwa katika Chati Na.19.





**Chati Na. 19**: *Ulinganifu wa utendaji kwa shule za mijini na vijijini katika kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa.*

Chati Na.19 inaonesha kuwa asilimia 39.42 ya wanafunzi wa shule za vijijini walikuwa na utendaji hafifu wakati asilimia 34.77 ya wanafunzi wa shule za mijini walikuwa na utendaji

hafifu. Hii inadhihirisha kuwa, uwezo wa wanafunzi wa kujibu maswali ya Kujumlisha na Kutoa ni mzuri zaidi kwa shule za mijini kuliko vijijini.

### 4.7.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri wa Kutambua Namba na Kufumbua Mafumbo Kimikoa

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika upimaji wa kujibu kwa kuandika uliofanyika katika kutambua namba na kufumbua mafumbo kwa kila mkoa umefanyika. Ulinganifu huo umezingatia idadi ya wanafunzi walioweza kujibu kwa usahihi maswali yasiyopungua 6 kati ya 10 ambao ni utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Vile vile, wanafunzi waliojibu maswali yasiyozidi 4 kwa usahihi walikuwa na utendaji hafifu. Ulinganifu wa utendaji umefanyika katika mikoa 26 yenye jumla ya wanafunzi 28,022 walifanya upimaji huo. Matokeo ya ulinganifu huo yameoneshwa kwenye Chati Na. 20.





**Chati Na. 20:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mikoa.*

Katika Chati Na. 20, uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mikoa unaonesha kuwa kati ya mikoa 26, mikoa 5, ambayo ni Morogoro, Dar es Salaam, Ruvuma, Dodoma na Njombe ilikuwa na kiwango cha juu cha utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 88.08, 82.81, 77.01, 74.20 na 73.96 mtawalia. Kwa ujumla, wanafunzi wengi katika mikoa mingi walikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu. Hata hivyo, wanafunzi katika mikoa mitano ambayo ni Rukwa, Kigoma, Songwe, Katavi na Shinyanga walikuwa na kiwango cha juu cha utendaji hafifu kwa asilimia 53.85, 51.14, 48.78, 48.11 na 46.20 mtawalia.

### 4.7.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Upimaji wa Umahiri wa Kujumlisha na Kutoa Namba kwa Kuzingatia Mikoa

Katika upimaji wa umahiri wa kujumlisha na kutoa, wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kwa mdomo. Jumla ya wanafunzi 28,816 walipimwa katika upimaji huo. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji katika mikoa 26 ya Tanzania Bara umeoneshwa katika Chati Na. 21.





**Chati Na. 21:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia mikoa.*

Chati Na. 21 inaonesha kuwa wanafunzi katika mikoa 5 kati ya mikoa 26, ambayo ni Geita, Mbeya, Dar es Salaam, Ruvuma na Mwanza walikuwa na kiwango cha juu cha utendaji wa wastani hadi mzuri sana cha asilimia 80.63, 74.28, 74.28, 73.52 na 71.38, mtawalia. Kwa upande mwingine, wanafunzi katika mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Kigoma, Iringa na Mtwara ilikuwa na kiwango cha juu cha utendaji hafifu cha asilimia 58.24, 48.89, 45.07, 44.75 na 44.53, mtawalia, ikilinganishwa na mikoa mingine. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na uwezo wa kujibu kwa usahihi maswali yaliyopima umahiri wa kujumlisha na kutoa namba nzima hadi 999.

### 4.7.5 Ulinganifu wa Wanafunzi kwa Ujumla Kimikoa

Ulinganifu wa jumla wa utendaji wa wanafunzi waliopimwa katika kila mkoa katika stadi ya Kuhesabu umefanywa katika sehemu hii. Ulinganifu huo ulifanywa kwa kuzingatia wanafunzi waliopata kuanzia alama 13 mpaka 50. Aidha, ulinganifu huo umefanyika kwa mikoa yote 26 yenye wanafunzi 28,022 ambao walifanya upimaji. Matokeo ya upimaji yameoneshwa katika Chati Na. 22.




**Chati Na. 22:** *Ulinganifu wa jumla wa utendaji wa wanafunzi kimikoa.*

Chati Na. 22 unaonesha kuwa wanafunzi katika mikoa 5 kati ya 26, ambayo ni Morogoro, Dar es Salaam, Ruvuma, Dodoma na Pwani walikuwa na utendaji wa juu ambao ni asilimia 87.30, 83.20, 76.71, 75.50 na 73.50, mtawalia. Katika mikoa hiyo, wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Kwa upande mwingine, wanafunzi wa mikoa ya Rukwa, Kigoma, Mara, Songwe na Katavi walikuwa na utendaji hafifu wa asilimia 41.50, 49.40, 52.50, 53.90 na 54.60, mtawalia ikilinganishwa na mikoa mingine. Hii inaonesha kuwa mikoa yote ilikuwa na utendaji mzuri na mzuri sana katika Stadi ya Kuhesabu.

## 4.8 Muhtasari wa Uchambuzi Katika Stadi ya Kuhesabu

Katika upimaji wa Stadi ya Kuhesabu maswali yalipima viwango vya utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mfululizo, Kufumbua Mafumbo yaliyohusu kujumlisha na kutoa namba nzima, Kujumlisha na Kutoa.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kutambua namba inayokosekana kwenye mfululizo wa namba, asilimia 69.52 na 52.27 ya wanafunzi waliweza kubaini kwa usahihi namba zinazokosekana katika mfululizo wa namba zinazoongezeka kwa 1 na 10, mtawalia. Aidha, katika mfululizo wa namba zinazopungua kwa 1, asilimia 38.08 ya wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi. Hata hivyo, katika mfululizo wa namba zinazoongezeka kwa 5, ni asilimia 23.74 tu ya wanafunzi walioandika jibu sahihi. Pia, katika mfululizo wa namba zinazoongezeka kwa 2, ni asilimia 20.65 tu ya wanafunzi waliandika jibu sahihi. Wanafunzi wengi walikuwa na utendaji wa chini kwa kukosa maarifa na ujuzi wa kutosha, hasa katika mfululizo wa namba zenye tarakimu mbili.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kujumlisha, asilimia 64.69 ya wanafunzi walionesha kuwa na uelewa mzuri katika kujumlisha namba yenye tarakimu moja kwenye namba yenye tarakimu mbili bila kubeba na asilimia 53.05 katika kujumlisha namba yenye tarakimu moja kwenye namba yenye tarakimu mbili kwa kubeba. Pia, asilimia 45.29 ya wanafunzi waliweza kujumlisha kwa usahihi namba zenye tarakimu mbili bila kubeba. Hata hivyo, katika maswali ya kujumlisha namba zenye tarakimu mbili kwa kubeba, asilimia 26.43 na 23.58 walijibu kwa usahihi swali la 5 na 4, mtawalia.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kutoa, asilimia 56.08 na 47.02 ya wanafunzi walijibu kwa usahihi swali la kutoa namba yenye tarakimu moja kutoka kwenye namba yenye tarakimu mbili bila kukopa na swali la kutoa namba yenye tarakimu moja kutoka kwenye namba yenye tarakimu mbili kwa kukopa, mtawalia. Vile vile, wanafunzi walikuwa na utendaji wa asilimia 47.02 katika kutoa namba zenye tarakimu mbili bila kukopa. Katika maswali ya kutoa namba zenye tarakimu mbili kwa kukopa, asilimia 19.25 na 18.80 ya wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi swali la 10 na 9, mtawalia.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kufumbua mafumbo, asilimia 62.00 na 54.39 ya wanafunzi walifumbua kwa usahihi mafumbo yaliyohusu kujumlisha na kutoa namba zenye tarakimu moja, mtawalia. Aidha, asilimia 28.15 ya wanafunzi waliweza kufumbua kwa usahihi fumbo lililohusu kutoa namba zenye tarakimu mbili bila kukopa, na asilimia 19.01 fumbo lililohusu namba zenye tarakimu mbili kwa kukopa. Wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa usahihi kulisababishwa na kukosa maarifa na ujuzi wa kufumbua mafumbo yanayohusu kujumlisha au kutoa hasa namba zenye tarakimu mbili, kushindwa kubaini mahitaji ya mafumbo hivyo kutofumbua mafumbo hayo au kuandika majibu yasiyohusiana na fumbo husika.

Kwa ujumla, asilimia 64.20 ya wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi maswali ya upimaji wa Stadi ya Kuhesabu. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri katika upimaji huo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uwezo wa; kutambua namba inayokosekana katika mfululizo wa namba, kujumlisha namba zenye tarakimu moja na namba zenye tarakimu mbili kwa kubeba, kutoa namba zenye tarakimu moja na namba zenye tarakimu mbili kwa kukopa, kufumbua mafumbo kwa usahihi na kutumia kwa usahihi zana za kuhesabia kama vile karatasi na penseli, vidole na kutali. Kwa upande mwingine, asilimia 35.80 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu kutokana na; kukosa umahiri wa kusoma na kuandika namba, kutokuwa na uwezo wa kujumlisha kwa kubeba na kutoa kwa kukopa, kushindwa kufumbua mafumbo na kushindwa kutumia kwa usahihi zana za kuhesabia kama vile karatasi na penseli, vidole na kutali.

# SURA YA TANO

## HALI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KKK SHULENI

Madodoso yalitumika kupata taarifa kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Lengo la madodoso hayo lilikuwa kubaini hali halisi ya mazingira ya kufundishia na kujifunzia, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, walimu na rasilimali nyingine. Pia, inatoa ushauri wa jinsi ya kufanya maboresho mazuri.

### 5.1 Taarifa za Shule kwa Ujumla

Wakuu wa shule waliojaza madodoso walikuwa asilimia 491 sawa na asilimia 93.7. Uchambuzi wa madodoso unaonesha kuwa, walimu wa shule wapatao 309 (62.9%) walipata mafunzo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji KKK. Pia, walieleza kuwa walikuwa na idadi ya wanafunzi 40 na wasiozidi 50 kwa darasa.

### 5.2 Hali ya Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Wakuu wa shule walitakiwa kutoa taarifa kuhusu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia kama vile vitabu vya kiada na ziada. Hali ya upatikanaji wa vifaa na zana imewasilishwa katika Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na.9: Hali ya Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

| Na | Hoja | Idadi | % |
|---|---|---|---|
| 1. | Upatikanaji wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kuhesabu. | 468 | 95.3 |
| 2. | Upatikanaji wa vitabu vya ziada vya mazoezi ya Stadi ya Kuhesabu. | 431 | 87.8 |
| 3. | Uwepo wa vifaa vya kufundishia Stadi ya Kuhesabu kama vile vihesabio n.k. | 440 | 89.6 |
| 4. | Uwepo wa vifaa vya Kufundishia Stadi ya Kuandika kama vile vibao n.k. | 393 | 80 |
| 5. | Uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kusoma. | 471 | 95.9 |
| 6. | Upatikanaji wa vifaa vinavyolenga kuendeleza Stadi ya Kusoma, kama vile vitabu vya hadithi fupi. | 467 | 95.1 |

**N = 491**

Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa, kwa ujumla, kiwango cha vifaa vya kufundishia kilikuwa kizuri kwa Stadi zote kama ilivyoelekezwa katika muhtasari wa Darasa la I na la II. Vitabu vya kiada, ziada na vifaa vingine kwa ajili ya Stadi zote tatu vilikuwa na upatikanaji mzuri kwa zaidi ya asilimia 95.9.

Takwimu pia zinaonesha kuwa Stadi ya Kusoma ilikuwa na vitabu vingi zaidi vya kiada na ziada kama vile vitabu vya hadithi fupi, ambavyo vilikuwa na asilimia 95.9 na 95.1, mtawalia. Aidha, upatikanaji wa vitabu vya kiada, ziada na vihesabio kwa Stadi ya Kuhesabu ulikuwa mzuri kwa asilimia 89.6. Katika Stadi ya Kuandika, kulikuwa na uhaba wa vifaa hivyo ikilinganishwa na Stadi nyingine (80.0%). Hata hivyo, kwa maelezo ya baadhi ya wakuu wa shule kiwango kilichopo kinakidhi na wanafunzi wanajifunza vizuri ingawa kuna nafasi ya kusambaza vitabu zaidi ili kuziba pengo la upungufu lililopo.

## 5.3 Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji KKK

Kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, wakuu wa shule walijibu vipengele vyote kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10: Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji**

| Na. | Hoja | Idadi | % |
|---|---|---|---|
| 1. | Uwepo wa madawati, viti na meza za kutumia walimu wa Darasa la I na la II shuleni | 445 | 90.6 |
| 2. | Hali ya uwepo wa vyumba vya madarasa ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa Darasa la I na la II waliopo shuleni. | 367 | 74.7 |
| 3. | Upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa ajili ya kunywa wanafunzi pamoja na usafi binafsi kama vile kunawa mikono wanapotoka chooni. | 382 | 77.8 |
| 4. | Mahusiano na ushirikiano kati ya uongozi wa shule, walimu na wazazi/walezi wa wanafunzi wa Darasa la II. | 467 | 95.1 |

**N = 491**

Takwimu katika Jedwali Na. 10 zinaonesha kuwa kulikuwa na uhusiano mzuri kati ya uongozi wa shule na wazazi ambapo asilimia 95.1 ya wakuu wa shule waliridhika na hali iliyopo. Kuhusu upatikanaji wa huduma ya maji shuleni, asilimia 77.7 ya wakuu wa shule zilizofanyiwa upimaji waliripoti upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Uchambuzi wa madodoso umebainisha kuwa asilimia 90.6 ya wakuu wa shule zilizoshiriki upimaji waliripoti uwepo wa utoshelevu wa samani maalum zinazowezesha ufundishaji na ujifunzaji wa KKK kufanyika kwa ufanisi. Hata hivyo, samani hizo zilikuwa zikitumika katika madarasa yenye msongamano (25.3%), kwani asilimia 74.7 ya wakuu wa shule ndio walioripoti kuwa na madarasa ya kutosha. Pamoja na uwepo wa samani hizo, baadhi ya wakuu wa shule waliibua hoja kuwa samani kama vile madawati na viti haziendani na umri wa wanafunzi, zinaonekana ni ndefu zaidi kuliko wao, hivyo kusababisha kushindwa kukaa vizuri. Pia, asilimia 36.7 ya shule zilizofanyiwa upimaji majengo yake hayakuwa katika hali nzuri.

Japokuwa kulikuwa na upungufu wa majengo na samani, shule nyingi (66.6%) ziliweza kukidhi ukaaji wa wanafunzi 40 katika chumba kimoja cha darasa kama ilivyoelekezwa katika mtaala wa elimu ya msingi Tanzania wa mwaka 2007. Kwa nyongeza, asilimia 84.7 ya wakuu wa shule walikuwa na vyumba vya madarasa vinavyotosheleza kukaa wanafunzi wasiozidi 50.

## 5.4 Vikwazo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK

Wakuu wa shule walitakiwa kueleza vikwazo vya utekelezaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa KKK katika miktadha yao. Vikwazo hivyo vimeainishwa katika Jedwali Na.11.

**Jedwali Na. 11: Vikwazo katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za KKK**

| Na. | Hoja | Idadi | % |
|---|---|---|---|
| 1. | Umbali wa wanafunzi kutoka nyumbani hadi shuleni. | 275 | 56.0 |
| 2. | Mahudhurio yasiyoridhisha. | 262 | 53.4 |
| 3. | Uhaba wa walimu wa Stadi za KKK. | 352 | 71.7 |
| 4. | Kupokea wanafunzi wanaohamia wenye stadi za KKK zisizoridhisha. | 238 | 48.5 |
| 5. | Uhaba wa vitendea kazi vya kufundishia na kujifunzia, kama vile vitabu n.k | 263 | 53.6 |

**N = 491**

Kama Jedwali Na. 11 linavyoonesha, umbali wanaotembea wanafunzi toka nyumbani hadi shule unaathari katika ujifunzaji wa wanafunzi kwa

uchovu, njaa na kiu ya maji. Changamoto hii iliathiri zaidi mikoa ya Simiyu na Katavi ambapo wakuu wa shule 17 katika mikoa hiyo waliiona kama changamoto kubwa. Mikoa mingine ilikuwa Singida na Iringa iliyotajwa na idadi ya wakuu wa shule 16 na 14, mtawalia.

Changamoto nyingine ni mahudhurio ya wanafunzi yasiyoridhisha (53.4%), na ambayo yalielezewa kuwa yalitokana na hali ngumu ya maisha katika familia na ujinga. Pia, baadhi ya shule zilijengwa katika maeneo yasiyo rafiki kwa mwanafunzi kwenda na kurudi shuleni. Mwisho, kulikuwa na upungufu wa walimu wa kufundisha KKK ambao ulitajwa na asilimia 53.6 ya waliojibu dodoso.

# SURA YA SITA

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.1 Hitimisho

Kwa ujumla uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi katika stadi zote (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) kwa wanafunzi wa darasa la pili 2019 ulifanyika kikamilifu. Uchambuzi huu ulihusisha Shule za Serikali zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Katika Stadi ya Kusoma, wanafunzi 21,554 (74.80%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kutokana na umahiri wao wa kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha na kasi inayotakiwa. Vilevile wanafunzi hao walionesha umakini mkubwa kwa kusoma tena kifungu hicho kwa kukielewa, kukitafsiri kisha kujibu maswali ya ufahamu. Hata hivyo, wanafunzi 7,263 (25.22%) walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kusoma maneno yaliyoundwa na silabi zenye muundo wa konsonanti mwambatano, kutokuweza kutamka sauti zilizounda maneno mbalimbali katika sehemu sahihi za matamshi, kushindwa kusoma kwa ufasaha na kasi inayotakiwa na kuathiriwa na lugha ya asili katika usomaji wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Vilevile, hawakuwa na umahiri wa kusoma kifungu cha maneno kwa kukielewa, kukitafsiri kisha kujibu maswali ya ufahamu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 21,670 (75.20%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika Stadi ya Kuandika. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuunda herufi na maneno. Vilevile, waliweza kutambua picha na kuandika majina ya picha husika na kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo. Hata hivyo, waliweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. Kwa upande mwingine, wanafunzi 7,279 sawa na asilimia 24.80 walikuwa na utendaji hafifu kwani walishindwa kuandika majina ya picha, kubainisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo na kushindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi.

Aidha, katika Stadi ya Kuhesabu wanafunzi 17,991 (64.20%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Wanafunzi hao, walikuwa na uwezo wa kujumlisha kwa kubeba, kutoa kwa kukopa kutumia zana za kuhesabia kama vile, vidole, kutali penseli na karatasi. Hata hivyo,

wanafunzi 10,031 (35.80%) walikuwa na utendaji hafifu kwa kuwa walikosa umahiri wa kusoma na kuhesabu, uwezo wa kujumlisha kwa kubeba na kushindwa kutumia zana za kuhesabia.

Ulinganifu kati ya shule za mjini na vijijini unaonesha kuwa shule za mjini zilikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 80.28 kuliko shule za vijijini ambazo zilikuwa na asilimia 72.47. Hii inatokana na shule za mijini kuwa na walimu wengi pamoja na miundombinu ya kutosha, hivyo kuwawezesha kuwapa wanafunzi maarifa yote yaliyopo katika mihtasari ya masomo husika.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa utendaji wa wanafunzi katika Stadi zote tatu (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) kwa kuzingatia mikoa, mkoa uliokuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ni Dar- es salaam ambapo ulikuwa na asilimia 92.58. Aidha, mkoa wa mwisho katika stadi hiyo ni mkoa wa Kigoma kwa kuwa na asilimia 59.77. Aidha, katika Stadi ya Kuandika, mkoa uliokuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ni Morogoro, ambapo ulikuwa na asilimia 93.58. Aidha mkoa wa mwisho katika stadi hiyo ni Kigoma ambapo ulikuwa na asilimia 51.89, na katika Stadi ya Kuhesabu mkoa uliokuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana ni Morogoro ambapo ulikuwa na asilimia 88.08. Aidha mkoa wa mwisho katika stadi hiyo ni mkoa wa Rukwa ambapo ulikuwa na asilimia 53.85.

Kwa ujumla, uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi kimkoa unaonesha kuwa mkoa wa Kigoma umeshika nafasi ya mwisho katika Stadi mbili za Kusoma na Kuandika. Hata hivyo, katika Stadi ya Kuhesabu mkoa huo umeshika nafasi ya pili kutoka mwisho. Hivyo, juhudi za maksudi zinahitajika ili kuimarisha na kuongeza utendaji mzuri wa wanafunzi katika mikoa iliyokuwa katika kiwango kibaya na cha wastani.

## 6.2 Mapendekezo

Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi katika Stadi zote tatu ulibaini changamoto mbalimbali. Ili kuondoa changamoto na kuongeza zaidi utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza kuwa:

(a) Walimu wanaofundisha Stadi ya Kusoma watilie mkazo katika kuwaongoza wanafunzi kusoma maneno hamsini (50) kwa ufasaha na kasi inayotakiwa (dakika moja), hasa kusoma

maneno yenye konsonanti mwambatano na kuhakikisha wanafunzi wanatamka sauti mbalimbali mahala sahihi pa matamshi. Aidha, kuwaongoza wanafunzi kusoma vifungu vya maneno kwa ufasaha, kuelewa na kutafsiri walichokisoma ili kujibu kwa urahisi maswali ya ufahamu.

(b) Walimu wanaofundisha Stadi ya Kuandika waweke msisitizo na mazoezi ya kutosha katika kutambua picha mbalimbali, kuandika herufi mwambatano, na kuunda silabi na maneno. Vilevile, walimu wawaelekeze wanafunzi kutambua maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo na kunakili vifungu vya maneno pamoja na kujua kutumia alama za uandishi.

(c) Ili kuboresha Stadi ya Kuhesabu, walimu wafundishe kwa kutumia zana za kufundishia kama vile, vihesabio. Aidha, watoe mazoezi ya kutosha katika kukamilisha mfuatano wa namba, kujumlisha kwa kubeba, kutoa kwa kukopa na kufumbua mafumbo.

(d) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kupitia Idara ya Udhibiti Ubora wa shule na Uongozi wa Elimu ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shule wafuatilie ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ili kuzifanyia kazi changamoto zilizobainika.

## Kiambatisho Na. 1: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kusoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA PILI

STADI YA KUSOMA NA KUHESABU

KARATASI YA MWANAFUNZI

Muda: Dakika 20 Ijumaa, 31 Januari 2020 asubuhi

Maelekezo

1. Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali **yote kwa mdomo**.
2. Kila mwanafunzi atapimwa kwa **dakika 20**.
3. Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi juu ya fomu maalum ya upimaji kwa **kalamu ya wino wa bluu**.
4. Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma na kujibu maswali ya ufahamu na kuhesabu, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika skeli ya upimaji kwa kutumia **kalamu ya wino mwekundu.**

Ukurasa wa 1 kati ya 4

Tina na Subira ni marafiki. Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

1. 11 + 6 =
2. 15 + 8 =
3. 11 + 23 =
4. 27 + 36 =
5. 42 + 18 =

6. 17 - 3 =
7. 20 - 8 =
8. 35 - 24 =
9. 46 - 19 =
10. 50 - 21 =

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA DARASA LA PILI STADI YA KUSOMA NA KUHESABU**
**KWA KUTUMIA TABLET (KISHIKWAMBI)**

**SEHEMU A**

**201 STADI YA KUSOMA**

1. Kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha, umakini na kasi inayotakiwa. (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

**Gusa** kila neno ambalo mwanafunzi atashindwa kulisoma na neno hilo litakuwa na rangi **nyekundu**. Iwapo uligusa neno ambalo mwanafunzi alikosea kusoma na akarudia kusoma kwa usahihi, **gusa tena** neno hilo na rangi nyekundu itaondoka.

(a) Mweleke̱ze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika **tablet**.

(b) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma neno baada ya **sekunde 3**, mweleke̱ze kusoma neno linalofuata.

(c) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma **maneno yote** ya sentensi ya kwanza kishikwambi kitasitisha zoezi hivyo endelea na stadi ya kuhesabu.

(d) Iwapo mwanafunzi atasema **sijui** wakati akisoma neno, chukulia kama ni **kosa**.

(e) Iwapo mwanafunzi atashindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya **sekunde 60**, **gusa (hold)** kwa muda neno la mwisho alilosoma mwanafunzi.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

Karibu ..........Hujambo?

(a) Hapa kuna kifungu cha maneno, nikisema anza utasoma (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na kwa haraka kadri uwezavyo.

(c) Weka kidole kwenye neno la kwanza. Je uko tayari? Anza.

2. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

(a) Mwongoze mwanafunzi kusoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe kwa kugusa kwa kalamu **kuanzia** sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari). Baada ya mwanafunzi kusoma ndani ya **dakika 3**, chukua karatasi ya mwanafunzi kisha muulize maswali yaliyopo kwenye **tablet**.

(b) Mwanafunzi akitoa jibu sahihi gusa alama ya **vema** (√), iwapo atatoa jibu lisilo sahihi gusa alama ya **kosa** (X). Endapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi na kisha kufanya marekebisho kwa kutoa jibu sahihi gusa alama ya **vema** (√).

(c) Iwapo mwanafunzi ataulizwa swali na kushindwa kujibu ndani ya **sekunde 10**, utatakiwa kugusa alama ya **kosa** (X) kisha kuendelea na swali linalofuata.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Utasoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari).

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na kwa haraka kadri uwezavyo. Baada ya kusoma nitachukua karatasi yako kisha nitakuuliza maswali yanayotokana na kifungu cha maneno ulichosoma. Je upo tayari? Anza.

## SEHEMU B

## 203 STADI YA KUHESABU

**Maelekezo kwa Msimamizi**

Gusa alama ya **vema** (√) kwenye **tablet** endapo mwanafunzi atajibu kwa usahihi swali husika au alama ya **kosa** (X) iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi. Iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi na kisha kufanya marekebisho kwa kutoa jibu sahihi gusa alama ya **vema** (√).

(a) Mwongoze mwanafunzi kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa. Mpe karatasi na penseli kisha mwambie kuwa anaweza kutumia kama anataka lakini sio lazima.

(b) Iwapo mwanafunzi atatumia njia isiyoridhisha muulize kama anaweza kutumia njia nyingine.

(c) Iwapo mwanafunzi ataendelea kutumia njia isiyoridhisha au atasimama/atakwama/hatajibu kwa **sekunde 5** kisha endelea na swali linalofuata.

(d) Sitisha zoezi endapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kujumlisha kisha endelea na maswali ya kutoa.

(e) Iwapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kutoa sitisha zoezi. Endelea na mwanafunzi anayefuata.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Hapo kuna maswali ya kujumlisha na kutoa (mwoneshe mwanafunzi kwa mkono swali la 1 hadi la 5 kisha swali la 6 hadi 10).

(b) Utaanza na swali la 1. Utajibu maswali hayo kwa mdomo. Unaweza kutumia penseli na karatasi kama unataka lakini sio lazima. Je upo tayari? Anza.

## Kiambatisho Na. 2. Skeli ya Upimaji Stadi ya Kusoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

Fomu Maalum ya Kujaza Alama za Mwanafunzi katika Upimaji wa Kusoma na Kuhesabu

Jina la Mwanafunzi______________________________

Namba ya Mwanafunzi______________________________

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| STADI YA KUSOMA | | | STADI YA KUHESABU | | |
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| | | | 1. | | |
| | | | 2. | | |
| 1. | | | 3. | | |
| | | | 4. | | |
| | | | 5. | | |
| | | | 6. | | |
| | | | 7. | | |
| 2. | | | 8. | | |
| | | | 9. | | |
| | | | 10. | | |
| Jumla ya Alama | | | | | |

Ukurasa wa 1 kati ya 7

CC-2020-XXX

## SEHEMU A

201 **STADI YA KUSOMA**

1. Kusoma kifungu cha maneno kwa ufasaha, umakini na kasi inayotakiwa. (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma kwenye kifungu cha maneno. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kusoma kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 00½**)

(a) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha maneno kilichopo katika **Skeli ya Upimaji**.

(b) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma neno baada ya **sekunde 3** mwelekeze kusoma neno linalofuata.

(c) Iwapo mwanafunzi atashindwa kusoma **maneno yote** ya sentensi ya kwanza, sitisha zoezi na weka alama ya mabano [ ] katika neno la mwisho kusomwa kisha endelea na stadi ya kuhesabu.

(d) Iwapo mwanafunzi atasema **sijui** wakati akisoma, chukulia kama ni **kosa** kisha weka alama ya mkwaju.

(e) Iwapo mwanafunzi atashindwa kumaliza kusoma kifungu cha maneno ndani ya **sekunde 60**, weka alama ya mabano [ ] katika neno la mwisho alilosoma.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

Karibu ..........Hujambo?

(a) Hapa kuna kifungu cha maneno, nikisema anza utasoma (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari).

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na kwa haraka kadri uwezavyo.

(c) Weka kidole kwenye neno la kwanza. Je uko tayari? Anza.

Tina na Subira ni marafiki.

Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Alama:** ☐ **Muda uliotumika:** ☐

2. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama 25).

**Maelekezo kwa Msimamizi**

(a) Mwongoze mwanafunzi kusoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari. Baada ya mwanafunzi kusoma ndani ya **dakika 3**, chukua karatasi ya mwanafunzi kisha muulize maswali yaliyopo kwenye **Skeli ya Upimaji**.

(b) Mwanafunzi akitoa jibu sahihi zungushia alama **5**, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama **0**. Endapo mwanafunzi atatoa jibu lisilo sahihi na kisha kufanya marekebisho kwa kutoa jibu sahihi, weka mkwaju kwenye alama 0 kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali.

(c) Iwapo utamuuliza swali mwanafunzi na akashindwa kujibu ndani ya **sekunde 10**, zungushia alama 0 kisha endelea na swali linalofuata.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Utasoma tena kifungu cha maneno (mwoneshe mwanafunzi kwa kugusa kwa kalamu kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari).

(b) Utasoma maneno kwa sauti, umakini na kwa haraka kadri uwezavyo. Baada ya kusoma nitachukua karatasi yako kisha nitakuuliza maswali yanayotokana na kifungu cha maneno ulichosoma Je uko tayari? Anza.

Tina na Subira ni marafiki. Wanaishi kijiji cha Ng'alo. Kijiji chao kina shida kubwa ya maji. Siku moja, Tina na Subira walikwenda kisimani kuteka maji. Subira alichukua kata na kujaza ndoo yake. Mara akaanza kupiga kelele, kumbe alikuwa amechomwa na mwiba. Hatimaye, Subira alishindwa kubeba ndoo. Wazazi wake walimpeleka hospitali.

**Maswali na Majibu**

| Kipengele | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | Rafiki yake Tina anaitwa nani? **(Subira)** | 5 | 0 |
| 2. | Tina na Subira wanaishi katika kijiji gani? **(Ng'alo)** | 5 | 0 |
| 3. | Tina na Subira walikwenda wapi? **(Kisimani)** | 5 | 0 |
| 4. | Subira alitumia nini kujaza maji kwenye ndoo yake? **(Kata)** | 5 | 0 |
| 5. | Kwanini Subira alipelekwa Hospitali? **(Kwa sababu alikuwa amechomwa na mwiba/ kwa sababu alikuwa ameumia/ ili apate matibabu/ili apate dawa)** | 5 | 0 |
| **Jumla ya Alama** | | | |

## SEHEMU B

## 203 STADI YA KUHESABU

**Maelekezo kwa Msimamizi**

Zungushia alama **2** iwapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi, zungushia alama **0** iwapo atatoa jibu lisilo sahihi. Iwapo mwanafunzi atatoa jibu lisilosahihi na kisha kufanya marekebisho na kutoa jibu sahihi, weka mkwaju kwenye alama **0** kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali.

(a) Mwongoze mwanafunzi kujibu maswali ya kujumlisha na kutoa. Mpe karatasi na penseli kisha mwambie kuwa anaweza kutumia kama anataka lakini sio lazima.

(b) Iwapo mwanafunzi atatumia njia isiyoridhisha muulize kama anaweza kutumia njia nyingine.

(c) Iwapo mwanafunzi ataendelea kutumia njia isiyoridhisha au atasimama/atakwama/hatajibu kwa **sekunde 5** kisha endelea na swali linalofuata.

(d) Sitisha zoezi endapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kujumlisha kisha endelea na maswali ya kutoa.

(e) Iwapo mwanafunzi atakosa maswali **manne ya mwanzo** katika maswali ya kutoa sitisha zoezi. Endelea na mwanafunzi anayefuata.

**Maelekezo ya Msimamizi kwa Mwanafunzi**

(a) Hapo kuna maswali ya kujumlisha na kutoa (mwoneshe mwanafunzi kwa mkono swali la 1 hadi la 5 kisha swali la 6 hadi 10).

(b) Utaanza na swali la 1. Utajibu maswali hayo kwa mdomo. Unaweza kutumia penseli na karatasi kama unataka lakini sio lazima. Je upo tayari? Anza.

| Na. | Maswali na majibu | Alama | |
|---|---|---|---|
| 1. | 11 + 6 = **(17)** | 2 | 0 |
| 2. | 15 + 8 = **(23)** | 2 | 0 |
| 3. | 11 + 23 = **(34)** | 2 | 0 |
| 4. | 27 + 36 = **(63)** | 2 | 0 |
| 5. | 42 + 18 = **(60)** | 2 | 0 |
| 6. | 17 - 3 = **(14)** | 2 | 0 |
| 7. | 20 - 8 = **(12)** | 2 | 0 |
| 8. | 35 - 24 = **(11)** | 2 | 0 |
| 9. | 46 - 19 = **(27)** | 2 | 0 |
| 10. | 50 - 21 = **(29)** | 2 | 0 |
| | **Jumla ya Alama** | | |

**Maoni ya msimamizi**

Weka alama ya vema (√) iwapo mwanafunzi:

☐ ametumia vidole au kutali.

☐ ametumia karatasi na penseli.

☐ amejibu maswali yote kwa kichwa.

## Kiambatisho Na. 3: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika

Jina la Mwanafunzi________________________
Namba ya Mwanafunzi______________________

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA DARASA LA PILI

202 STADI YA KUANDIKA

Muda: Dakika 40 Alhamisi, 30 Januari 2020 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **matatu**. (3).
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika **majibu yako yote** kwa kutumia penseli.
4. Andika **Jina lako** na **Namba yako** katika kila ukurasa.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| Jumla | | |

1 807005 1000013

Ukurasa wa 1 kati ya 4

Jina la Mwanafunzi________________________
Namba ya Mwanafunzi________________________

1. Tazama kwa makini picha zifuatazo kisha andika **majina yake** katika nafasi zilizo wazi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) |  ____________________ | (b) |  ____________________ |
| (c) |  ____________________ | (d) |  ____________________ |

Jina la Mwanafunzi________________________
Namba ya Mwanafunzi______________________

| | | | |
|---|---|---|---|
| (e) |  ________________ | (f) |  ________________ |
| (g) |  ________________ | (h) |  ________________ |
| (i) |  ________________ | (j) |  ________________ |



CC-2020-RAK

Jina la Mwanafunzi________________________
Namba ya Mwanafunzi______________________

2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa **herufi ndogo**.

(a) MVULANA, msichana, BABU, bibi

(b) NYANYA, KAROTI, pilipili, kitunguu

(c) dawati, KITI, meza, KABATI

(d) PAPAI, pera, NANASI, fenesi

(e) fisi, MBUZI, twiga, SUNGURA

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)**, na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Umeiona ile bustani yenye maua mazuri ___ Looh ___ inapendeza sana ___ pamoja na kuwa inahitaji kumwagiliwa maji mengi ___

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

## Kiambatisho Na. 4: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuhesabu

Jina la Mwanafunzi_______________

Namba ya Mwanafunzi _____________

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA PILI

203 STADI YA KUHESABU

Muda: Dakika 50 Alhamisi, 30 Januari 2020 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwa **penseli**.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | | 6. | | |
| 2. | | | 7. | | |
| 3. | | | 8. | | |
| 4. | | | 9. | | |
| 5. | | | 10. | | |
| Jumla ya Alama | | | | | |

1 8070005 100013

Ukurasa wa 1 ya kati 3

CC-2020/XXX

Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 3, 4, 5, ___, 7, 8.
2. 27, 26, 25, 24, ___.
3. 54, 56, 58, ___, 62.
4. 10, ___, 30, 40, 50.
5. 40, 45, ___, 55, 60.
6. Kikapu kina machungwa 3. Iwapo yataongezwa machungwa 2, kikapu hicho kitakuwa na machungwa mangapi?

   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________

7. Juma alikuwa na pipi 7. Alimpa rafiki yake pipi 4. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________

8. Daftari langu la Kuandika lina kurasa 48. Ikiwa kurasa 32 zimejaa, je, zimebaki kurasa ngapi ambazo hazijaandikwa?

   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________

9. Musa alinunua mayai 33 siku ya kwanza. Siku ya pili alinunua mayai 19. Je, jumla alinunua mayai mangapi?

10. Mwalimu alikuwa na penseli 51. Aliwapa wanafunzi penseli 17. Je, alibakiwa na penseli ngapi?